Nipashe
Alhamisi Januari 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580467
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Sababu** JPM kupewa tuzo Kiswahili hizi

UKURASA 3



**Ajichoma** moto hadi kufa kwa wivu wa mapenzi

UKURASA 3

**Zidane awakataa Alaba, Mbappe**

UKURASA 21

# Utata mzito wagubika kifo cha mwanafunzi

• **Mama** yake adaiwa kutaka kujiua kwa sumu, wadogo zake waibuliwa kwenye dimbwi maji ya mvua...

*Endelea Ukurasa 2*



Muuguzi wa Zahanati ya Mtana, wilayani Tarime, mkoani Mara, Rebeka Samson (kulia), akitoa huduma ya kliniki ya watoto chini ya mti katika Kijiji cha Nyagiswa, wilayani humo, mapema wiki hii, kutokana na kijiji hicho kukosa zahanati. **PICHA: DINNA STEFANO**

## YALIYOMO

UKURASA WA 19

### TRUMP AONDOKA, AJIVUNIA MAFANIKIO

RAIS wa Marekani, Donald Trump, jana aliondoka rasmi madarakani huku akitamba...

## Ukaguzi magari toka nje kufanyika nchini

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM



## Corona ilivyoibua ukiukwaji wa mtaala wa elimu shuleni

UKURASA 4

**MICHEZO** **KAZE: YANGA SC SASA RAHA TU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Utata kifo cha mwanafunzi Dar

**Na Maulid Mmbaga**

UTATA umegubika kifo cha mtoto Mariam Yakunga (17), ambaye haijajulikana kama amejinyonga au kunyongwa nyumbani kwao Mtaa wa Nike Tegeta A, Kata ya Goba jijini Dar es Salaam.

Wakati kukiwa na utata kuhusu kifo cha mwanafunzi huyo wa sekondari, mama yake anadaiwa kutaka kujiua kwa kunywa sumu, huku watoto wake wadogo wawili wakikutwa kwenye dimbwi la maji ya mvua.

Akizungumzia tukio hilo jana, jirani wa familia hiyo, Ahmed Abdallah, alisema tukio hilo limemshtua kwa kuwa miezi mitatu iliyopita, baba wa binti huyo Kalosi Yakunga, alifariki dunia akiacha mke na watoto watatu.

Jirani huyo alisema kuwa baada ya baba wa familia hiyo kufariki dunia, mkewe alikabidhiwa jukumu la kuilea na kwamba, Januari 18 mwaka huu, Mariam alitakiwa kurudi shule, lakini kutokana na matatizo ya kifamilia, hakufaulu kwa kiwango cha kumwezesha kuingia kidato cha nne katika shule aliyokuwa anasoma.

"Kwa sababu nilikuwa karibu sana na hii familia, mama wa binti huyo alinipa taarifa kuwa mtoto ameambiwa hawezi kuendelea na shule hiyo aliyokuwa anasoma kwa sababu ameshindwa kufikisha wastani wa asilimia 50, hivyo atafute shule nyingine," alifafanua.

Abdallah alisema mwanafunzi huyo pia alikuwa amekosa ada na mahitaji mengine muhimu ya shule na walikuwa wanashirikiana kumtafutia shule nyingine, lakini walikosa fedha za kulipia na kulazimika kubaki nyumbani.

Kwa mujibu wa Abdallah, mama wa mtoto alimjulisha kuwa anafuatilia mirathi na ikiwezekana auze baadhi ya mali walizoachiwa, ili watoto waende shule kwa kuwa tangu mumewe afariki dunia, hakuna msaada wowote aliopata kutoka kwa ndugu wa mumewe.

"Kwa bahati mbaya leo (jana) nilipokuwa ofisini, nilipokea taarifa kuwa mama wa familia ile amejiua pamoja na familia yake.

"Nilipofika eneo la tukio, tulibaini aliwatupa watoto wawili wadogo kwenye shimo la kuhifadhia maji ya mvua na tuliwatoa na kuwapeleka hospitali kwa ajili ya kufanyiwa matibabu na mtoto mkubwa ambaye ni Mariam tulikuta tayari ameshafariki.

"Tulijaribu kumtafuta mama wa familia hiyo na hatukumwona eneo la tukio na baada ya muda nilikuta 'missed call' ya namba ya huyo shemeji yangu na nilipopiga, alipokea mwanamume na kuniambia kuwa mwenye simu yupo Hospitali ya Palestina amekunywa sumu," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Ramadhan Kingai, alithibitisha kupokea taarifa ya tukio hilo na kubainisha kuwa bado wanaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo chake.

"Tumepokea taarifa ya tukio hilo na tunalifuatilia na taarifa itatoka kesho (leo) au keshokutwa (kesho) baada ya kubaini sababu iliyosababisha mtoto huyo kufariki dunia," alisema.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere (kulia), akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wa Kamati ya Bajeti, Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), wakati wa mafunzo kuhusu aina za ukaguzi unaofanywa na CAG, katika Ukumbi wa Msekwa Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Ukaguzi ubora wa magari kuanza kufanyika nchini

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema kuanzia sasa ukaguzi wa ubora wa magari yaliyotoka nje utafanyika nchini na kuwataka wananchi kufuata utaratibu wa sasa ili kuepuka usumbufu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano TBS, Roida Andusamile, magari hayo ni kutoka nje ya nchi na ukaguzi huo utaanza Machi Mosi, mwaka huu.

"Utaratibu wa kukagua magari kutoka nje ya nchi utafanyika baada ya kuwasili nchini, magari yote yatakayosafirishwa kuanzia Machi Mosi yatakaguliwa katika Bandari ya Dar es Salaam," alisema na kuongeza:

"Kwa sasa TBS inakagua magari kutoka nje ya nchi kupitia mawakala watatu kutoka Japan na mmoja kutoka Dubai, ambao mikataba yao itakoma hivi karibuni, hivyo vyeti vya ukaguzi vitakavyotolewa na mawakala tajwa kwa magari yatakayosafirishwa kuanzia Machi Mosi, havitatambuliwa TBS."

Kwa mujibu wa taarifa ya Roida, magari yatakayopimwa bandarini na kutokidhi matakwa ya kiwango yatahitaji kufanyiwa matengenezo nje ya bandari kisha kuletwa na kupimwa tena kwenye yadi ya UDA mkabala na Bandari ya Dar es Salaam.

"Shirika litaendelea kuhakikisha kuwa magari yote yaliyotumika na kuingizwa nchini yanakidhi matakwa ya kiwango cha magari yaliyotumika," alisisitiza.

## Serikali: Hatujapokea taarifa ya Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema haijapokea taarifa rasmi kutoka serikali ya Marekani kuhusiana na kuwekewa vizuizi vya kuingia nchini humo kwa baadhi ya maofisa wake wanaodaiwa kutia dosari demokrasia wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ndiyo iliyobainisha hayo jana, baada ya kuulizwa na Nipashe kuhusiana na tamko la Marekani kupitia Waziri wa Mambo ya Nje wa taifa hilo, Mike Pompeo, msemaji wa wizara hiyo, Emmanuel Buhohela, alisema hadi sasa hawana taarifa rasmi.

"Taarifa hiyo nimeiona kwenye mitandao ya kijamii kama ambavyo wewe (mwandishi) umeona, hadi sasa hakuna taarifa rasmi ya mawasiliano kati ya serikali na serikali, kwa kuwa kuna utaratibu maalum wa kuwasiliana," alisema Buhohela na kuongeza:

"Hatuwezi kuongea lolote juu ya hilo kwa kutumia taarifa za mtandaoni."

Katika ukurasa wa Twitter wa Pompeo, aliandika kuwa Marekani imeamua kuwawekea vikwazo vya kuingia nchini humo maofisa wa Tanzania ambao wanadaiwa kuharibu Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka jana.

Marekani ilidai maofisa hao (bila kuwataja), wanatajwa kuhusika kuingilia mchakato wa uchaguzi na kuminya utekelezaji wa demokrasia.

Mwaka jana Tume ya Taifa ya Uchaguzi Tanzania (NEC) ilimtangaza Rais John Magufuli kuwa mshindi kwa kura milioni 12.5 sawa na asilimia 84.4 na mshindani wake wa karibu wa Chama Kikuu cha Upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu akipata kura milioni 1.9 sawa na asilimia 13.04.

Kwa upande wa Zanzibar, Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), ilimtangaza Dk. Hussein Ali Mwinyi kupitia tiketi ya CCM kuwa mshindi kwa kupata asilimia 76.27 ya kura akifuatiwa na Maalim Seif Sharif Hamad kupitia tiketi ya ACT –Wazalendo aliyepata asilimia 19.87.

Aidha, waangalizi mbalimbali walisema kuwa uchaguzi huo ulikuwa huru na haki.

## HABARI KITAIFA

# Sababu JPM kutunukiwa tuzo Kiswahili zatajwa



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto), akikagua uunganishaji wa mabomba ya kupeleka maji kwa wananchi katika mradi wa maji wa bwawa la Matwiga, wilayani Chunya, mkoani Mbeya jana, ambao unatarajiwa kuwanufaisha wananchi wa vijiji 16. **PICHA: NEBART MSOKWA**

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Kiswahili Tanzania (BAKITA) limemtunuku Rais John Magufuli, nishani ya juu ya Shaban Robert, kwa kutambua mchango wake wa kukuza lugha ya Kiswahili ndani na nje ya mipaka ya nchi.

Akitoa maelezo mafupi juu ya nishani hiyo ya juu ya Shaban Robert, Mwenyekiti wa Bodi ya BAKITA, Dk. Methwel Samweli, alisema moja ya sababu za kumpatia nishani hiyo Rais Magufuli ni kutokana na utashi wake wa kisiasa kukuza Kiswahili.

Alisema katika kipindi cha utawala wake, Rais Magufuli amekuwa na mchango mkubwa katika kukuza Kiswahili ndani na nje ya mipaka ya nchi.

Vile vile, alisema sababu nyingine ni Rais Magufuli kutumia lugha ya Kiswahili katika mikutano yake ya nje na ndani ya nchi, hali ambayo imechangia kuongeza fursa ya lugha hiyo kujiuza.

"Rais amekuwa akitumia lugha ya Kiswahili anapokuwa ndani na nje ya nchi hali ambayo imesaidia kukikuza Kiswahili na kufungua fursa ya uwapo wa wakalimani wa lugha hiyo pamoja na ajira ya walimu wa lugha ya Kiswahili," alisema.

Pia alisema katika ziara ya Rais Magufuli aliyoifanya Zimbabwe na Namibia, alitumia lugha ya Kiswahili kuhutubia na kuonyesha nia ya kupeleka walimu wa lugha hiyo kufundisha katika nchi hizo.

"Lakini Rais Magufuli akiwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) alichangia Kiswahili kuwa lugha rasmi ya jumuiya kuungana na lugha za Kifaransa, Kireno na Kingereza," alisema.

Katika kuhitimisha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Sulemani Abdallah, alisema ili kukuza lugha ya Kiswahili juhudi zinahitaji kwa BAKITA na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA).

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kukuza Kiswahili ili kuwa bidhaa inayohitajika ndani na nje ya nje.

"Watanzania inatakiwa hivi sasa tutumie fursa hii ya lugha ya Kiswahili kuanzisha vituo vya kufundisha lugha ya Kiswahili katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika SADC," alisema.

Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Abdalah Ulega, alisema kuwa serikali itahakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakuwa bidhaa muhimu na inayohitajika ndani na nje ya nje.

"Tutahakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa sehemu ya kuzalisha ajira kwa Watanzania na kila anayejua lugha hiyo kunufaika nayo," alisema Ulega.

# Ajichoma moto hadi kufa madai ya wivu wa mapenzi

**Na Hamisi Nasri,** NEWALA

MKAZI wa Mtaa wa Julia, Newala mkoani Mtwara, Hashim Selemani, maarufu kama Chikwisu, amefariki dunia baada ya kujimwagia mafuta ya petroli mwilini na kujichoma moto hadharani.

Tukio hilo lililotokea juzi mchana mjini hapa, linadaiwa kuhusishwa na wivu wa kimapenzi.

Mtoto wa marehemu aliyejitambulisha kwa jina la Msafiri Hashim, alisema baba yake amefariki dunia baada ya kujimwagia mafuta ya petroli kisha kujiwasha moto na kusababisha majeraha makubwa katika mwili wake na hatimaye kufariki dunia.

Alisema kuwa chanzo cha baba yake kuchukua hatua hiyo ya kujichoma moto ni ugomvi kati yake na mke wake juu ya ndoa yao. Takribani wiki moja iliyopita, ilidaiwa Selemani alimfumania mke wake akiwa na mwanamume mwingine.

Hashim alisema baada ya tukio hilo, mke wake hakuwa sawa kisaikolojia hadi juzi alipoamua kuchukua uamuzi huo kutafuta mafuta kisha kujimwagia na kujichoma moto.

Alisema baada ya baba yake kufanya tukio, familia ilipata taarifa na kwenda sehemu ambayo alikuwa amefanyia kitendo hicho na kumkuta amejeruhiwa vibaya na moto sehemu mbalimbali za mwili.

Kwa mujibu wa Hashim, baada ya kumkuta katika hali hiyo, familia ilimchukua na kumpeleka Hospitali ya Misheni Ndanda wilayani Masasi kwa ajili ya matibabu, lakini walipofika hapo alikuwa ameshafariki dunia.

"Nimesikitishwa sana na tukio hili la baba yangu kujichoma moto. Kwa kweli baba alikuwa ngunzo muhimu katika familia yetu. Tulimkimbiza hospitalini lakini kutokana na majeraha makubwa aliyokuwa ameyapata mwilini, alifariki dunia," alisema Hashim.

Alisema mke wake baada ya kusikia mume wake amejichoma moto na kufariki dunia, aliamua kutoweka na kwenda kusikojulikana na kwamba familia tayari imeshatoa taarifa polisi juu ya tukio la marehemu kujichoma moto.

Akizungumzia kutokea kwa tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Julia, Abdallah Mpende, alisema wanandoa hao walishawahi kufikia ofisini kwake baada ya mwanamume huyo kumfumania mke wake moja wiki iliyopita na kwamba ugomvi huo waliumaliza kwa kusuluhisha.

Alisema baada ya ofisi yake kuumaliza ugomvi huo, wanandoa hao walitoka ofisini hapo wakiwa wameelewana na kwamba baada ya hapo hakuwafuatilia mpaka aliposikia mume amejichoma moto na kufariki dunia.

Mganga wa zamu wa Hospitali ya Ndanda aliyeupokea mwili wa marehemu, Swaumu Zuberi, alisema mgonjwa huyo alifikishwa hospitalini hapo akiwa na majeraha makubwa ya kuungua sehemu za kuanzia kichwani mapaka maeneo ya tumboni.

Alisema baada ya kumpokea madaktari walipambana kuhakikisha wanaokoa maisha yake, lakini kwa bahati mbaya alifariki dunia kwa sababu ya majeraha makubwa aliyekuwa ameyapata mwilini mwake.

Jeshi la Polisi mkoani Mtwara limethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba linaendelea kumtafuta mke wa marehemu aliyekimbilia kusikojulikana baada ya kusikia mume wake amejichoma moto.


**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS) 2021-01-21**

TANZANIA BUREAU OF STANDARDS tbs

**TAARIFA KWA WAAGIZAJI WA MAGARI KUTOKA NJE YA NCHI**

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linawataarifu waagizaji na wauzaji wa magari kutoka nje ya nchi kuwa kuanzia tarehe 01 mwezi Machi, 2021, utaratibu wa kukagua magari kutoka nje ya nchi utafanyika baada ya kuwasili hapa nchini (Destination Inspection).Hivyo,magari yote yatakayosafirishwa kuanzia tarehe tajwa hapo juu yatakaguliwa katika bandari ya Dar-es-Salaam.

Kwa sasa TBS inakagua magari kutoka nje ya nchi kupitia mawakala watatu(3) kutoka Japan na mmoja(1) kutoka Dubai ambao mikataba yao itakoma hivi karibuni.

Hivyo vyeti vya ukaguzi vitakavyotolewa na mawakala tajwa kwa magari yatakayosafirishwa kuanzia tarehe 01 mwezi Machi, 2021 havitatambulika na TBS.

Aidha,magari yatakayopimwa bandarini na kutokidhi matakwa ya kiwango yatahitaji kufanyiwa matengenezo nje ya bandari na kisha kuletwa na kupimwa tena kwenye yadi ya UDA mkabala na Bandari ya Dar es salaam.
Shirika litaendelea kuhakikisha kuwa magari yote yaliyotumika na kuingizwa nchini yanakidhi matakwa ya kiwango cha magari yaliyotumika.
Kwa taarifa zaidi kuhusu utaratibu huu mpya usisite kuwasiliana na:-

Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Viwango Tanzania (TBS),
SLP 9524,
Dar es Salaam.
Simu: +255(022)2450298/Hotline: +0800110827
Barua pepe: **info@tbs.go.tz/Tovuti: www.tbs.go.tz**
**malalamiko @tbs.go.tz**

RIPOTI MAALUM

# Corona ilivyoibua ukiukwaji wa mtaala wa elimu shuleni

● Pia kiulizo haki za walimu kisheria

Na Mwandishi Wetu

VIRUSI vya corona vilivyoripotiwa kulipuka Wuhan, China Desemba 2019, vimekuwa na madhara karibu kwa kila sekta ulimwenguni.

Hadi jana saa saba mchana, mtandao wa Worldmeters ulionyesha kulikuwa na watu 96,701,903 waliopata maambukizo huku 2,067,951 wakifariki dunia kutokana na virusi hivyo.

Nchini kumebainika kuwapo ukiukwaji mkubwa wa kanuni na miongozo ya taaluma kwa baadhi ya shule za binafsi, zinazobadilisha taratibu wa ufundishaji ili kufidia muda uliopotea wakati wa mlipuko wa virusi hivyo.

Nipashe imebaini baadhi ya wanafunzi, hasa wanaokabiliwa na mitihani, wanakalishwa darasani wakifundishwa kuanzia alfajiri hadi usiku.

Pia adha hiyo ya muda wa ziada unagusa kufutwa kinyemela kwa mapumziko ya wikiendi, siku ya Jumamosi na baadhi ya shule hata Jumapili, kufanywa kuwa za mahudhurio darasani.

Udadisi wa Nipashe katika baadhi ya shule za jijini Dar es Salaam umebaini mpango wa muda wa ziada unatokana na kufidia miezi mitatu (wiki 13 au wastani saa 78), ambao watoto hawakuwapo masomoni kutokana na mlipuko wa maradhi ya corona Machi, mwaka jana.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Wamiliki wa Shule na Vyuo binafsi (TAMONGSCO), Benjamin Nkonya, akizungumza na gazeti hili, anatetea nyongeza ya muda huo kwamba ni kufidia muda uliopotea wa masomo, kutokana na adha ya corona.

"Mwanafunzi anatakiwa kukaa siku 194 kwa mwaka, zimepungua mwaka jana (2020) kutokana na corona, hii inafidia siku zilizopungua miezi mitatu.

"Wazazi wakubaliane na hiyo hali, hata kulipa ada yote mbali na shule kufungwa sababu huduma ziliendelea kwenye shule mfano ulinzi, maji," anasema Nkonya.

Hata hivyo serikali iliagiza shule zote kuongeza muda wa saa mbili za masomo darasani kufidia muda uliopotea wanafunzi walipokuwa nyumbani.

Katika kipindi cha miezi sita ambacho walihudhuria masomo kuanzia Juni 29 mwaka jana hadi Desemba 18, ambayo inamaanisha kuondoa likizo fupi ya zaidi ya wiki moja, Agosti mwaka jana, wanafunzi wamehudhuria darasani kwa wastani wiki 22.

Kwa kuzingatia mahudhurio shuleni ya siku tano kwa wiki, wanafunzi wamekaa darasani kwa siku 110, ambayo kila siku ya masomo walikuwa na saa mbili za ziada inayowapa jumla ya saa 220 wakati zilizopotea kwa corona zilikuwa saa 78, hivyo kuna ziada isiyopungua saa 140, sawa na wiki 20.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako.

Uchunguzi wa Nipashe, uliozuru katika shule mbalimbali za wilaya za Kinondoni, Ubungo, Ilala na Temeke, umebaini msukumo mkuu nyuma ya pazia kwa tishio hilo la kiafya kwa wanafunzi, ni ushindani wa kibiashara.

Baada ya kubainika ufaulu ndiyo mvuto mkuu wa soko kwa shule, nazo kutokana na ushindani mkubwa uliopo, zimejikuta zikitumia mbinu kwa mfumo wa kuigana kibiashara.

Uchunguzi wa Nipashe, baadhi ya shule zilizoko maeneo ya Ubungo, Kimara, Ukonga, Mbezi Beach, Tabata, Segerea na Mbagala, umebaini wanafunzi wengi wa darasa la saba na la nne wamekuwa wakiingizwa darasani kuanzia alfajiri hadi kati ya saa mbili na saa tatu pasipo kurudishwa bwenini.

Shule nyingi zimegundulika kuwalazimisha wanafunzi wa madarasa yanayokabiliwa na mitihani, zaidi darasa la nne na la saba, pia kidato cha pili na cha nne wanahamishiwa mabwenini kwa malipo ya ziada maradufu.

Ni hatua ambayo baadhi ya wazazi waliohojiwa na Nipashe, akiwamo Bryson Eliezer na Hilda Mosha (majina ya watoto wao na shule wanakosoma tunayo), wamethibitisha wameshawishiwa kupeleka bwenini watoto wao, ili wakasaidiwe kwa karibu kitaaluma, pasipo kuwekewa wazi mengine yanayojiri kuhusu ratiba.

**MAELEKEZO YA KISERIKALI**

Ratiba hiyo inapingana na maelekezo kutoka Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2007, unaoweka wazi muda wa kusoma au kujifunza kwa aliyeko kuanzia darasa la tatu hadi la saba, ukomo wake ni saa sita kwa siku.

Aidha, serikali inaelekeza kwa wanafunzi walioko katika madarasa ya kwanza na la pili, wasizidishe saa tatu na nusu (3½) kila siku.

Vivyo hivyo, serikali inaelekeza kila mwaka wa masomo utakuwa mihula miwili itakayokuwa na majuma 21 kwa kila muhula.

Hiyo inamaanisha kila muhula utakuwa na jumla ya siku 147, ambayo ni sawa na wastani wa miezi mitano kasoro siku kadhaa.

Hali kadhalika, ikirejewa maagizo ya mwanafunzi wa darasa la tatu hadi la saba, anatakiwa kukaa muda wa saa sita akisoma na kujifunza, kwa anayeingia asubuhi walau hadi saa tisa muda wake utakuwa umeisha, tena kwa maelekezo ya kati ya Jumatatu hadi Ijumaa.

Serikali inaelekeza kila wiki madarasa ya tatu hadi saba, ambayo yanaangukia kwenye makundi ya mitihani, yatakuwa na jumla ya vipindi 42 yenye dakika 40 kila kimoja.

Lakini kwa kile Nipashe imekibaini, ufundishaji umefikisha si chini ya vipindi 84 hadi 90 kwa wiki.

**SHIDA YA AFYA**

Daktari wa Binadamu, Pedro Pallangyo, akizungumza na gazeti hili, anasema kiafya saa za kukaa darasani kwa mtoto aliye shule ya msingi zisizidi 12.

"Kila kitu kina kipimo chake, saa 12 kwa mtoto wa shule ya msingi, hapana! Ubongo hauwezi kupokea kwa saa zote hizo," anasema Dk. Pedro.

Mtaalamu wa Lishe, Theresia Thomas, ana msisitizo wake kuhusu hilo kwamba kadri mwanafunzi anavyotumia muda mrefu katika masomo darasani, atahitaji chakula kilicho na nishati ya kutosha kipindi cha mapumziko.

"Kikubwa nishati lishe inahitajika kuzingatiwa kwa mtoto yeyote. Iwapo mzazi ataona ni vyema akamfungashia mtoto wake juisi au matunda, ili akipata muda ale, muda wa mapumziko itafaa na si kusoma saa nyingi bila mlo, uelewa unachangiwa na lishe," anasema Theresia.

Msaikolojia Tiba, Saldin Kimangale, anasema kumrundikia mtoto mambo mengi, anaangukia kupata msongo wa mawazo na hofu, inayomwondoa hatimaye katika hamasa na kufurahia masomo.

"Kumjazia mtoto mambo mengi na hasa ratiba zao za shule kiasi cha kukosa wakati wa kucheza na kufurahi ni kasoro katika malezi bora.

Mtaalamu huyo, anataja athari anazoweza kuzipata kutokana na kujaziwa mambo mengi kwa wakati mmoja ni pamoja na kupoteza vipaji na ubunifu alivyonavyo.

"Afya ya mwili ya mtoto pia huathirika, na kama tujuavyo afya ndio rasilimali na mtaji wa kila tunachofanya," anakumbusha mtaalamu huyo.

**SHERIA YA MTOTO**

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inatamka wazi kwamba wazazi hawana budi kuwapeleka watoto shuleni na kuwapa nafasi ya kucheza na kupumzika.

Wakati kukiwa na ukukwaji wa haki za wanafunzi kwa kukalishwa darasani muda wa ziada kuanzia mapema asubuhi hadi usiku kati ya saa tatu na nne kwa shule nyingi za watu, nako kumezaa kiulizo kwenye haki za walimu wanaowafundisha.

Wakati inaelekezwa kisheria wanafunzi wanapaswa kuhudhuria masomo kwa wastani wa muda usiozidi saa saba, Sheri ya Ajira na Uhusiano Kazini, iliyoanza nchini mwaka 2004, inaweka wazi muda wa mfanyakazi kutumika ni saa tisa kwa siku.

Vilevile, ina ufafanuzi pindi inapotokea muda wa ziada, usizidi saa mbili na nusu. Lakini, inaporejea uhalisia wa kilichotokea baada ya mlipuko wa corona na kinachoendelea sasa baada ya shule kufunguliwa, ratiba za masomo zinachukua saa 14 kwa siku.

Ni mustakabali unaozua kiulizo kuhusu 'utii bila shuruti' wa sheria za nchi, waraka rasmi na maelekezo ya kiserikali, hata wanafunzi wakakaa darasani mara mbili ya muda uliolekezwa na serikali, huku walimu wao wakiwa na wastani wa ziada ya saa tatu hadi nne kazini.

**KAULI YA WAZIRI ELIMU**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako, hivi karibuni katika mkutano mkuu wa mwaka wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania Bara (TAHOSSA), ana hoja inayojibu kinachojiri.

"Kumeibuka tabia ya shule imesajiliwa kama ya kutwa mara ya muda kidogo inakuwa ya bweni bila hata kufuata taratibu eti tuu kwa sababu imejenga 'kajengo kamoja na kukaita' bweni.

"Darasa la mitihani ndiyo walimu wanaona ndilo la kumjazia mtoto vitu vyote, unakuta hata shule hawafungi eti tu kwa sababu ya mitihani kwa nini hali hiyo isiwe toka madarasa mengine ya chini na siyo kusubiri wakati wa mitihani?" Anahoji Ndalichako.

Agizo la Prof. Ndalichako, ambaye ni mtaalamu bingwa wa mitaala, anazitaka shule binafsi zirejee na kuhakikisha hazitoki nje ya kanuni za usajili wao na kuacha tabia ya kujichukulia hatua bila kuishirikisha serikali.

Vivyo hivyo, anaelekeza kidole cha kung'aka dhidi ya tabia za shule kusubiri darasa la mitihani, ndiyo wanahamia utaratibu wa kuwalimbikizia masomo wanafunzi.

# Majaliwa: Tukirejesha mkonge tutaokoa bil. 577/- kila mwaka

**Na Lulu George,** TANGA

KUFUFUA zao la mkonge kutaiwezesha Tanzania kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 577 zinazotumika kuagiza vifungashio kutoka nje ya nchi kila mwaka.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hatua inayochukuliwa hadi sasa na serikali, imeingiza mkonge katika orodha ya mazao nyeti ya kimkakati, na hadi sasa Tanzania ni mzalishaji mkuu wa pili duniani, ikitanguliwa na Brazil.

Akizungumza jana katika kikao cha wadau wa zao la mkonge na kushirikisha wakulima, wafanyabiashara na viongozi kutoka mikoa mitano inayolima mkonge nchini, Majaliwa alisema mpaka kufikia mwaka 2025, Tanzania inatarajia itazalisha tani 120,000 za mkonge kwa mwaka.

Alisema ufufuaji wa zao hilo ambalo ni moja ya mazao ya kimkakati yanayolengwa na serikali katika kuongeza pato na taifa na kukuza uchumi, pia unatarajiwa kuwezesha serikali kuongeza fedha za kigeni.

Waziri Mkuu alisema Tanzania inatumia Dola za Marekani milioni 245 hadi 250 (Sh. bilioni 577.277) kwa ajili ya kuagiza vifungashio kutoka nje ya nchi kila mwaka.

Majaliwa alisema kwa sasa Tanzania ni nchi ya pili katika uzalishaji wa mkonge kwenye soko la dunia ikitanguliwa na Brazil inayozalisha tani 150,000 kwa mwaka.

Alisema zao la mkonge ni miongoni mwa mazao ya biashara nchini ambayo mikakati yake ikitekelezwa vizuri, itawezesha serikali kupata fedha za kigeni na kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja.

Alisema serikali katika kutambua hilo iliongeza zao la mkonge la mchikichi katika idadi ya mazao ya mkakati ambayo ni korosho, pamba, kahawa, tumbaku na chai.

"Kilimo cha mkonge na mchikichi kinatuondolea mzigo mkubwa sana kwa kupunguza gharama, mfano baada ya kuhamasisha kulima mchikichi, tunaokoa zaidi Dola za Marekani milioni 470 kuagiza mafuta kutoka nje ya nchi," alisema.

Waziri Mkuu aliagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha wanazalisha vitalu vya miche ya mkonge na kuwapatia wakulima.

Aliitaja mikoa mitano inayolima mkonge kuwa ni pamoja na Tanga, Kilimanjaro, Pwani, Morogoro, Mara na Shinyanga.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wizara imeandaa utaratibu wa hati ya dhamana (LC)utakaowezesha wakulima wadogo kuchukua mkopo kwenye taasisi za fedha kwa riba ya asilimia mbili.

Kutokana na hilo, Bashe alizitaka halmashauri zinazolima mkonge, kuhakikisha zinatumia utaratibu huo na kuwezesha vijana kwa kutumia asilimia 10 ya fedha zinazotolewa na halmashauri kama mkopo kuwawezesha kulima mkonge.

"Katika suala la mbegu kupitia taasisi zetu za utafiti ikiwamo TARI, ASA na TOSCI kumekuwa na uzalishaji wa mbegu ili kuongeza ubora wa miche na ubora wa zao la mkonge," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mkonge, Saadi Kambona, alisema kwa sasa mkulima mdogo ndiyo anayeongoza uzalishaji wa mkonge kwa kuzalisha tani 9,728 kupitia mashamba ya bodi hiyo.

Kambona aliwataja wazalishaji wengine kuwa ni Amboni anayezalisha tani 8,277 na Mohamed Enterprises anayezalisha tani 4,922.

Mkurugenzi huyo alisema bodi hiyo katika kipindi cha miezi 11 imekusanya zaidi ya Sh. milioni 300 kulinganishwa na Sh. milioni 84 zilizokuwapo awali.

"Wakati tunakabidhiwa ofisi, tulikuta Sh. milioni 84 tu, lakini baada ya kuanza kazi katika kipindi cha miezi 11, tumeweza kukusanya zaidi ya Sh. milioni 300, hivyo hatua yetu ni nzuri na tunao uwezo wa kuongeza uzalishaji na kumpita mshindani wetu ambaye ni Brazil," alisema.

Mpaka sasa eneo linalolima mkonge kwa Tanzania ni hekta 54 wakati Brazil wanalima hekta 10.

# LHRC yatoa neno viongozi kupiga watu viboko

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimekemea tabia ya baadhi ya viongozi kujichukulia sheria mkononi ikiwamo kuwapiga wananchi wanaotuhumiwa kwa makosa mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa ya kituo hicho kwa vyombo vya habari jana, iliyotiwa saini na Mkurugenzi Mtendaji wake, Anna Henga, hali hiyo inadidimiza ustawi wa haki za binadamu.

"Ni wazi kuwa tabia ya viongozi katika ngazi mbalimbali kujichukulia sheria mkononi imeshamiri hususani vitendo vya vipigo kwa wananchi wenye tuhuma za makosa ya jinai. Hali hii inazidi kudidimiza ustawi wa haki za binadamu.

"Pia inadidimiza misingi ya utawala bora nchini kwa mujibu wa viwango vya kimataifa hususani mkataba wa haki za kiraia na kisiasa wa mwaka 1966 pamoja na kitaifa kama ilivyowekwa katika Katiba," iliema taarifa hiyo.

Kituo hicho kilitoa wito kwa serikali kuchukua hatua za makusudi kudhibiti vitendo hivyo.

"LHRC inatoa wito kwa serikali kuchukua hatua za makusudi kudhibiti vitendo hivyo ikiwamo kukemea, kusimamisha, kutengua, uteuzi wa viongozi mara moja pale yanapotokea matukio ya aina hiyo. Tuhuma zozote za makosa ya jinai au madai zinapaswa kuwasilishwa katika vyombo vya kisheria.

"Ibara ya 13 ya Katiba inaweka haki kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria na wana haki ya bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa. Inaeleza wazi kuwa ni mahakama pekee ndicho chombo cha utoaji haki, viongozi na wananchi wana jukumu kubwa la kulinda amani ya nchi kwa kufuata sheria na Katiba walioapa kuilinda," iliongeza taarifa hiyo.

Pia LHRC ilimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Harrison Kamoga, kwa kuchukua hatua ya kumsimamisha kazi Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Hydom, aliyemshambulia mwananchi.

Mtendaji huyo wa kijiji aliyefahamika kwa jina la Adella Kente, anadaiwa kumshambulia mwananchi wa kijiji hicho cha Hydom, Rose Danielson, Januari 12, mwaka huu, kwa tuhuma za kutolipa michango ya kijiji.

Matukio ya baadhi ya viongozi kuwachapa hadharani watu wanapokosea yamekuwa yakisambaa katika mitandao ya kijamii hivi karibuni.

Hivi karibuni, kwa mfano, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kennan Kihongosi, aliwachapa viboko wananchi na wazazi wa watoto waliodaiwa kuiba vifaa vya ujenzi wa shule na madawati na kufanya chuma chakavu.


MBEYA CEMENT
COMPANY LIMITED

## EXPRESSION OF INTEREST
## PROVISION OF GOODS, SERVICE AND MINOR WORKS

**MBEYA CEMENT COMPANY LIMITED (MCCL)** is a subsidiary of the LafargeHolcim Group with its industrial operations based in Songwe, Plot No. 1 Industrial Area, Mbeya. MCCL is proud to offer an exciting opportunity for experienced and suitably qualified suppliers to provide spare parts and services for its 2021-year requirements. MCCL invites all interested companies to participate in expression of interest for provision of goods, services and minor works at MCCL company site as per below list of Lots.

| | | | |
|---|---|---|---|
| LOT No.01 | Supply of Vie belts | LOT No.19 | Supply of Welding Electrodes |
| LOT No.02 | Supply of Bearings | LOT No.20 | Air condition Maintenance services |
| LOT No.03 | Vehicle Maintenance (Garage services) | LOT No.21 | Fire extinguisher maintenance services |
| LOT No.04 | Supply of Vehicle Tires | LOT No.22 | Compressor maintenance services |
| LOT No.05 | Supply of Conveyor Belts and Idlers | LOT No.23 | Courier Services |
| LOT No.06 | Supply of Industrial Gases and LPG | LOT No.24 | Supply of Mechanical Consumables |
| LOT No.07 | Kiln Brick Lining services | LOT No.25 | Supply of Electrical Consumables |
| LOT No.08 | Plumbing Services | LOT No.26 | Supply of Stationaries |
| LOT No.09 | Minor civil works and maintenance | LOT No.27 | Burner Pipe Maintenance and Repair |
| LOT No.10 | Ball mill Maintenance | LOT No.27 | Scaffolding Erection |
| LOT No.11 | Satellite Cooler Maintenance and repair | LOT No.28 | Box conveyor Maintenance and repair |
| LOT No.12 | Welding and Fabrication works | LOT No.29 | Motor Rewinding Services |
| LOT No.13 | Conveyor belts Replacement | LOT No.30 | Bucket elevator Maintenance repair |
| LOT No.14 | Open gear Maintenance | LOT No.31 | Limestone crusher Overhaul |
| LOT No.15 | Hired Labour (Skilled & Unskilled) | LOT No.32 | Filter bags replacement |
| LOT No.16 | Industrial Fan Maintenance and repair | LOT No.33 | HGG Brick lining and Repair |
| LOT No.17 | Filter bags Maintenance | LOT No.34 | Hire of Crane /Lifting Equipment |
| LOT No.18 | Weighbridge Maintenance and Repair | LOT No.35 | Chain Conveyor Maintenance Repair |

**Interested companies meeting following minimum requirements should respond to this EOI:**

1. A minimum of three (03) years' experience in provision of selected Lot(s)
2. Compliance to all statutory requirements for running the business
3. Certification of dealership or distributorship (if any)
4. Financial capability.

**Interested Suppliers are requested to submit the following documents while responding to this EOI:**

- Letter of interest clearly indicating the above LOT no. reference(s), and years of experience in similar provision of goods, services or works.
- Copy Company Profile
- Copies of Business licenses and relative certifications and registrations (if any)

Interested companies that meet the minimum requirements and have the capacity to undertake any of the above-mentioned Lots, should express their interest by sending together with all documents requested to the email address **mcc.tender@lafargeholcim.com** on or before 13:00 hours East African Time (EAT), on 27th January 2021.

Companies satisfactorily meeting the above minimum requirements will receive a detailed pre-qualification questionnaire for further evaluation by Company.

Note: Only shortlisted companies/contractors shall receive call for Invitation For Tender

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Fursa za Kiswahili ni nyingi, tuzichangamkie*

**LUGHA** ya Kiswahili ina fursa nyingi ambazo zikitumika vizuri, zinaweza kuwanufaisha Watanzania wengi.

Pamoja na lugha ya Kiswahili kuwa ya Taifa tangu baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1964, bado fursa zake hazijatumika ipasavyo katika kuinufaisha nchi yetu na wananchi wake.

Umekuwapo uhamasishaji ambao umekuwa ukifanywa na viongozi wa serikali pamoja na wadau wengine, lakini kimsingi, Watanzania hatujazitumia fursa za lugha hiyo.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili yamekuwa yakiongezeka kutokana na kasi kubwa ya maendeleo duniani, ambayo kwa kiwango kikubwa yamechochewa na utandawazi.

Kukua kwa sayansi na teknolojia kumeifanya dunia sasa kuwa sawa na kijiji. Kwa maneno mengine, kwa sasa hakuna nchi inayoweza kujitenga na kujiita kisiwa, vinginevyo itaachwa na kubakia yenyewe.

Maendeleo hayo yameongeza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nchi nyingi, hivyo kuendelea kuongeza wigo katika mahitaji yake.

Awali lugha hiyo ilikuwa ikitumika kwa kiwango kidogo katika mataifa jirani ya Afrika Mashariki, lakini kwa sasa mataifa hayo na mengine nje ya ukanda huo yameanza kuitumia sana na mahitaji yanazidi kuongezeka kila uchao.

Jinsi mahitaji yake yanavyozidi kuongezeka na kuvuka mipaka, hivyo kuwa fursa katika maendeleo, serikali imeliona hilo na kutoa msimamo.

Hatua hiyo ilitangazwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye ametoa maagizo matano ya kimkakati ya matumizi ya Kiswahili, ikiwamo kuwapo kwa sera ya lugha hiyo.

Aliagiza kuhakikisha kumbukumbu zote muhimu za nchi zinatolewa kwa lugha ya Kiswahili.

Akifungua maadhimisho ya Siku ya Kiswahili nchini juzi, Samia alisema ili kufanikisha matumizi ya lugha hiyo, ni lazima matumizi yake yapangwe na kuratibiwa.

Alisema Kiswahili kina fursa nyingi za kiuchumi, kijamii na kisiasa duniani, na kuagiza kwamba kwa wizara zote mbili na mabaraza na taasisi zingine za kuendeleza Kiswahili kwamba hadhi ya sasa ya Kiswahili kikanda na kimataifa inachagiza kuwapo kwa mageuzi.

Aliagiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na wizara hiyo kwa upande wa Zanzibar, kukaa na wataalamu na kubaini maeneo na nyaraka za kiserikali ambazo bado Kiswahili hakitumiki ili hatua zichukuliwe.

Aliipongeza Wizara ya Katiba na Sheria ambayo imeanza kuchukua hatua kuhakikisha hukumu za mahakama zinatolewa kwa Kiswahili ili kuhakikisha wananchi wanyonge wanapata haki zao.

Aliagiza pia wizara hizo kushirikisha wadau wengine kuandaa mikakati ya kutangaza, kufundisha na kuendeleza lugha hiyo nje ya nchi.

Pia wizara zije na mkakati wa kuandaa wataalamu mbalimbali wa Kiswahili wakiwamo wakalimani, watafsiri, walimu na wengine ambao Tanzania itaanza kuwatumia kimkakati katika kukieneza Kiswahili.

Alisema taasisi za kuendeleza Kiswahili kama BAKITA na BAKIZA nazo sasa zikumbukwe kwa kupatiwa wataalamu na rasilimali fedha za kutosha ili kutekeleza jukumu hili la kimkakati la kukiendeleza Kiswahili, ikiwamo ni kuimarisha kitengo cha uchapaji na uchapishaji cha TUKI pamoja na kampuni za uchapishaji lengo ni kuhakikisha machapisho ya Kiswahili yanawafikia watu wengi wa ndani na nje ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## *Nimependa namna wanaolima pamba wanavyobebwa msimu huu*

**PAMBA** ni miongoni mwa mazao mata-no ya kimkakati, ambayo serikali imeamua kuyawekea mkazo maalum kuyaendeleza, pia kuyatafutia masoko, ili wakulima wanufaike na yenyewe ikipata kodi.

Ni orodha ambayo pia inajumuisha korosho, kahawa, chai na tumbaku, kukitarajiwa yote yataongeza mapato ya wakulima na kuwa chanzo cha kuaminika cha malighafi katika uchumi wa viwanda kitaifa.

Kwa muda mrefu wakulima wa pamba nchini, wamekuwa na malalamiko ya kutolipwa fedha zao kwa wakati na mizani ya kupima zao hilo kuchakuliwa hata wasipate haki stahili inayowafaa.

Mengine wanayolalamikiwa yanagusa kuuziwa mbolea feki na kukatwa fedha baada ya kuuza pamba, ili kulipia pembejeo zinazokopeshwa wakati wanapoandaa mashamba, hadi hatua ya kuvuna.

Katika jitihada za serikali kuwapunguzia kero wakulima wa zao hilo, iliamua kutopanga bei ya pamba katika msimu wa mwaka 2020, ili kuliwezesha soko kuamua na mkulima kupata mahali pa hakika kuuzia.

Badala yake, ndiyo ikabeba jukumu kuwa msimamizi mkuu anayehakikisha maslahi ya wakulima wa pamba yanalindwa muda wote, ili wapate soko la uhakika linalozingatia ushindani uliopo, kuwapa faida.

Ni hatua serikali inaitaka kutaka kufanya kilimo kuwa cha kibiashara na si kujikimu katika kuwaondolea wakulima vikwazo vinavyoweza kukwamisha juhudi zao za kuendeleza mazao au katika mustakabali huo.

Maana yake ni kwamba, wakulima waliokopeshwa viuatilifu, hawatakatwa fedha wakati wa kuuza pamba yao, kama ambavyo imezoeleka, kwa kuwa serikali itatumia utaratibu mwingine, ambao haumuumizi.

Hiyo inaweza kuwa habari njema kutoka kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika kikao cha wadau wa pamba mjini Bariadi, mkoa wa Simiyu.

Uamuzi huo uliotangazwa na serikali, unaweza kuwa moja ya mikakati yake ya kuendelea kilimo na mazao hayo ya kimkakati ya biashara, hivyo wakulima hawana budi kuchangamkia fursa hiyo.

Wakulima wa pamba au hata wa mazao mengine ya kimkakati, ni wajibu wao sasa kuchangamkia fursa hiyo, kwa kuwa inatarajiwa kuendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira na fedha za kigeni.

Serikali inasema yatakuwa yanauzwa kwa njia ya ushindani, huku wakulima wanaozalisha kwa ubora wakinufaika na bei ya juu zaidi, kwa lengo la kumuinua mkulima tajwa.

Serikali pia inasema, imepanga kuongeza usimamizi katika uzalishaji mazao hayo makuu ya biashara, kwa vile kwa kipindi kirefu ulishuka kutokana na matatizo mbalimbali.

Miongoni mwa matatizo yanayotajwa kuchangia hali hiyo ni kupungua tija katika uzalishaji, baadhi ya wakulima kuacha kulima mazao hayo, kutokana na kukata tamaa kwa sababu mbalimbali.

Baadhi ya sababu hizo ni viongozi wa vyama vya ushirika kutotekeleza vyema wajibu wao, wizi, dhuluma na ushiriki mdogo wa maofisa kilimo katika kusimamia kilimo cha kitaalamu.

Ni vyema sasa kama vyama vya ushirika vimeimarika, basi wakulima wakumbushwe kuuza pamba kupitia vyama hivyo ili kupunguza ulaghai kwenye mizani kwa kuwa wasimamizi na watumiaji wa mizani watakuwa ni wakulima wenyewe wa pamba na siyo mawakala.

Hivyo, wadau wote wa kilimo wakiwamo Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA), wanapaswa kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kutambua mizani feki na kuihakiki kabla ya msimu wa mwaka huu utakapowadia.

Elimu hiyo inaweza kuwasaidia kujilinda wenyewe, wakati maofisa vipimo wanapokosekana katika vituo vya kuuzia pamba yao. Pia ni namna ya kuwawezesha wakulima kupata faida ya thamani kamili ya jasho lao.

Kwa mikakati hiyo na mingine mingi, ni wazi kwamba, pamba ya Tanzania itarejesha hadhi yake ya kuitwa 'dhahabu nyeupe' na kuweza kutumika katika uimarishaji uchumi wa mkulima na nchi kwa ujumla.

# Serikali yatenga bilioni 4.2/- vituo uokoaji Ziwa Victoria

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

SERIKALI kupitia Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC), imepanga kujenga vituo sita vya kuratibu shughuli za ufuatiliaji na uokoaji katika Ziwa Victoria vitakavyogharimu Sh. bilioni 4.2.

Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Emmanuel Ndomba, alisema jana kuwa ujenzi wa vituo hivyo utaanza katika mwaka huu wa fedha katika maeneo ya Mwibara, Kakukuru, Nansio, Mwigobero, Ilemela na Magarini.

Alisema ujenzi wa vituo hivyo sita utakapokamilika, utasaidia katika shughuli za kutafuta na kuratibu shughuli za uokoaji pindi zinapotokea ajali Ziwa Victoria.

"Vituo hivyo ambavyo makao yake makuu yatakuwa wilayani Ilemela mkoani Mwanza, vitajengwa katika maeneo ya Mwibara, Kakukuru, Nansio, Mwigobero pamoja na Magarini.

"Ujenzi wa vituo hivyo sita utatekelezwa kwa gharama Sh. bilioni 4.2 zilizotolewa kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

"Vituo sita vya kuratibu shughuli za uokoaji katika Ziwa Victoria kwa upande wa Tanzania, ni miongoni mwa vituo 10 vitakavyojengwa katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda," alifafanua.

Ofisa Mfawidhi wa TASAC mkoani Geita, Rashid Katonga, aliwataka wamiliki wa boti kuzisajili kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi yao.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, Mkoa wa Geita unakadiriwa kuwa na zaidi ya boti 1,000 zinazotoa huduma ya usafirishaji katika Ziwa Victoria.

Hata hivyo, ofisa huyo alisema boti 750 zikiwamo za uvuvi na zinazosafirisha abiria na mizigo, ndiyo zimesajiliwa na hivyo kufanya kazi zake kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria.

"Kutosajiliwa kwa zaidi ya boti 250 kumeilazimu TASAC kutoa elimu kwa wamiliki wa boti kuhusu umuhimu wa kuthibitishwa kwa ubora wa vyombo husika," alisema.

# Arejeshewa nyumba aliyoporwa mikopo umiza

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, imemrejeshea Josephine Kiyuga, mkazi wa Viwanja vya Mwadui Manispaa ya Shinyanga, nyumba zake mbili ambazo alipokwa na kampuni ya mikopo umiza.

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Francis Luena, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wao wa kazi kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha wa 2020/21) huku akibainisha kuwa wameokoa Sh. milioni 10 pamoja na nyumba mbili.

Alisema mwanamke huyo alikopa Sh. milioni 5.5 kutoka kampuni ya ukopeshaji ya Mselikare na kutakiwa kurejesha Sh. milioni 7.7.

Katika mkataba wao wa kukopeshana, alisema mkopeshaji alichukua hati za nyumba mbili za mwanamke huyo na aliposhindwa kurejesha kwa wakati nyumba zake zikachukuliwa.

"Baada ya mwanamke huyu kuchukuliwa nyumba zake mbili, alijitahidi kumrejeshea Sh. milioni nane badala ya Sh. milioni 7.7 ikiwa ni ongezeko la Sh. 300,000 kama fidia ya riba ya kuchelewesha kulipa deni," alisema Luena.

"Mkopeshaji alipokea fedha hizo, lakini alikataa kurejesha hati za nyumba na kudai kuwa muda wa kurejesha deni ulishapita, hivyo kama mkopaji anahitaji nyumba zake, inabidi azinunue tena kutoka kwake kwa gharama ya Sh. milioni 19, ndipo akaja kwetu na tumemsaidia kupata nyumba zake," aliongeza.

Pia alisema wameokoa Sh. milioni 10 za wastaafu pamoja na wananchi ambao walidhulumiwa na waajiri wao na wameshawakabidhi fedha hizo.

Kiyuga alishukuru kwa kupata nyumba zake tena kwa kuwa alikuwa alishakata tamaa baada ya mkopeshaji huyo kuzing'ang'ania na kutaka kuziuza.



Mkuu wa Dawati la Uchunguzi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), mkoani Shinyanga, Emily Mandia (kulia), akimkabidhi mkazi wa viwanja vya Mwadui, Manispaa ya Shinyanga, Josephine Kiyuga, nyaraka za nyumba zake mbili ambazo zilitaifishwa na kampuni ya mkopo umiza ya Mselikare, baada ya kushindwa kurejesha mkopo kwa wakati Sh. milioni 7.7, alikopa Sh. milioni 5.5. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Wizara kuanza uhamasishaji Mpango Kabambe Dodoma

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inatarajiwa kuanza utekelezaji Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma kwa kuanza kuhamasisha wananchi wa kata za Mpunguzi na Matumbulu kufanya maendeleo kwa kuzingatia mpango huo.

Timu ya wataalamu wa wizara hiyo pamoja na Halmashauri ya Jiji la Dodoma ikiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Makazi Wizara ya Ardhi, Imaculate Senje, ilikutana na wenyeviti wa mitaa iliyo kwenye kata hizo kwa lengo la kuwajengea ufahamu kuhusiana na utekelezaji Mpango Kabambe.

Akizungumza na wenyeviti hao jana katika ofisi ya Mtendaji Kata ya Matumbulu jijini Dodoma, Imaculate, alisema wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, imeamua kuanza uhamasishaji wa utekelezaji wa mpango huo, ili wananchi wauelewe kuachana na dhana kwamba serikali inapora maeneo.

Mkurugenzi huyo Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Makazi aliongeza kuwa utekelezaji Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma unalenga maendeleo ya eneo hilo kufanyika kwa kuzingatia mpango huo.

Kwa mujibu wa Imaculate, kwa kuanzia utekelezaji Mpango Kabambe utaanzia Kata ya Mpunguni na kuhusisha maeneo ya mashamba na viwanda na baadaye katika maeneo ya makazi ya wananchi.

"Kipaumbele kwa sasa katika zoezi la utekelezaji Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma kitakuwa katika maeneo ya mashamba na viwanda na hapa tunataka tuepuke ujenzi holela katika maeneo hayo na kuzingatia mpango kabambe uliopo," alisema Imaculate.

Alisema kuwa wakati wa utekelezaji, hatua ya awali wataalamu watachukua taarifa za wamiliki wote kwenye maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya mashamba na viwanda na maeneo hayo yatapimwa na wamiliki wake kumilikishwa na kusisitiza kuwa, baada ya kumilikishwa, hawataruhusiwa kufanya maendelezo kinyume cha mpango kabambe.

**NAMPULA AUCTION MART AND COMPANY LTD**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA MARUDIO**

kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **BANK OF AFRICA (BOA)** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wao,ambayo ni nyumba iliyopo sinza kijiweni .

**Mnada utafanyika mahali nyumba ilipo tarehe 29/01/2021**

**Jina la mdaiwa:** ISSA MASOUD IDD
**Dhamana:** Nyumba
**Maelezo ya dhamana:** CT NO 19492 PLOT N0 336 BLOCK'C' SINZA AREA, L.O.NO 35471
**Tarehe ya mnada:** 29/01/2021

**Mashariti ya Mnada**
(a) Mnunuzi atalazimika kulipa 25%ya bei iliyofikiwa katika mnada papo hapo asilimia iliyobakia 75%italipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo.
(b) Endapo mnunuzi atashidwa kulipa asilimia 25% siku ya mnada basi mshindi wa pili ana haki ya kuweka hela siku hiyohiyo
(C) Mnunuzi akishidwa kutimiza sharti la 75% malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa
(d) Gharama za kubadilisha umiliki,kumtoa mtu kwenye nyumba na gharama nyingine zozote zitakazojitokeza itakuwa juu ya mnunuzi .gharama zozote zitakazo jitokeza nje ya utaratibu wa kibenki hatutahusika nazo

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA DALALI WA BENKI MOBILE: 0782 757829, 0712 050414/ 0719 441711**

**NAMPULA AUCTION MART AND COMPANY LTD**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu **NCBA BANK TANZANIA LIMITED** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wao,ambayo ni nyumba iliyopo **VINGUNGUTI AREA DAR ES SALAAM .**

**Mnada utafanyika mahali nyumba ilipo tarehe 06/02/2021**

**Jina la Mdaiwa:**
**Dhamana:** Nyumba
**Maelezo ya dhamana:** TITLE NUMBER 53982 LAND OF FICE NUMBER 203212 LAND PLOT 191/2/2 VINGUNGUTI AREA DSM
**Tarehe ya mnada:** 06/02/2021

**Mashariti ya Mnada**
(a) Mnunuzi atalazimika kulipa 25%ya beii liyofikiwa katika mnada papo hapo asilimia iliyo bakia .75%italipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo.
(b) Endapo mnunuzi atashidwa kulipa asilimia 25% siku ya mnada basi mshindi wa pili ana haki ya kuweka hela siku hiyohiyo .
(C) Mnunuzi akishidwa kutimiza sharti la 75% malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa
(d) Gharama za kubadilisha umiliki ,kumtoa mtu kwenye nyumba no gharama nyingine zozote zitakazoji tokeza itakuwa juu ya mnunuzi. .gharama zozote zitakazojitokeza nje ya utaratibu wa kibenki hatuta husika nazo

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA DALALI WA BENKI MOBILE:0782 757829, 0712 050414/ 0719 441711**

# Musoma watakiwa kuanzisha vikundi kupatiwa mikopo

**Na Sabato Kasika**

WAKAZI wa Musoma Vijijini mkoani Mara, wametakiwa kuanzisha vikundi vya kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara na kuvisajili kwenye halmashauri ili iwe rahisi kwao kuomba mikopo ya fedha, kwa ajili ya kuimarisha vikundi hivyo.

Wito huo ulitolewa juzi na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, na kufafanua kuwa zipo baadhi ya benki ziko tayari kutoa mikopo ya fedha kwenye vikundi ili kuinua uchumi.

"Tuanzishe vikundi vya kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara na kuvisajili katika halmashauri yetu na kuimarisha mitaji kwa kuomba mikopo ya fedha," alisema Prof. Muhongo.

Alisema, ingawa wakazi wa Musoma Vijijini kwa sasa wana majukumu mengi ikiwamo kushirikiana na serikali katika ujenzi wa madarasa ya shule shikizi, msingi na sekondari, bado anawakumbusha kujiimarisha kiuchumi.

Alisema, wananchi wamekuwa wakitumia nguvukazi zao na pia fedha taslimu, hivyo ili waendelee kuchangia ujenzi huo, hawanabudi kuimarisha vikundi kwa ajili kuinua uchumi wao ili waendelee kuchangia maendeleo.

"Wakati tukiwa katika majukumu hayo ambayo pia yanagusa afya kwa kujenga zahanati na vituo vya afya, ni muhimu pia tuongeze kasi kuunda vikundi vya uchumi viweze kutukomboa," alisema.



Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Umma, Peleleja Masesa (kulia), akipimwa VVU kwa hiari na Dk. Zainabu Mwinyi kutoka Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), wakati wa mafunzo kwa watumishi wa tume hiyo, kuhusu kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi mahala pa kazi, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mradi kunufaisha wajasiriamali kumiliki viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kamal katika kuunga mkono azma ya Rais John Magufuli ya kuwa na uchumi wa viwanda, imekuja na mradi wa kuwawezesha wajasiriamali wazawa 100 kumiliki viwanda vidogo vya kuchakata zao la korosho nchini badala ya kulisafirisha nje ya nchi kama malighafi.

Mwenyekiti wa Kamal, Gagan Gupta, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu azma hiyo itakayotekelezwa kupitia kampuni ya Kamal Agro Limited.

Alisema wazo hilo wamelipata baada ya utafiti uliofanyika takribani miaka mitano na kubaini ili kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa viwanda Tanzania, na kuja na mradi ambao utawawezesha Watanzania kutengeneza ajira kwa kuchakata bidhaa zinazozalishwa nchini Tanzania.

Gupta alisema mradi wa kuendeleza ujasiriamali wa kitaifa Tanzania katika sekta ya viwanda vya kuchakata korosho umenuia kutumia mbinu zinazotumika nchini India ili kuongeza thamani kwa korosho inayozalishwa nchini.

"Asilimia kati ya 70 na 80 ya korosho nchini India huchakatwa na viwanda vidogo vidogo kwa kushirikiana na viwanda vikubwa ambavyo husaidia wakati wa kuongeza thamani kabla bidhaa hazijapelekwa nje ya nchi kwa mauzo," alisema.

Alisema kupitia mpango huo wa uwezeshaji, wajasiriamali wa kitanzania watatengeneza maelfu ya ajira za moja kwa moja na kusaidia taifa kuokoa mamilioni ya Dola za Kimarekani zinazopotea kwa njia ya kuuza bidhaa ghafi nje ya nchi.

Gupta alisema mradi wa kuendeleza ujasiriamali wa kitaifa Tanzania katika sekta ya viwanda vya kuchakata korosho, umetengenezwa kwa namna ambayo kampuni hiyo itawapatia wajasiriamali wapatao 100 kila kitu wanachokihitaji ili kuendesha viwanda vidogo 100 vya kuchakata korosho.

"Mahitaji hayo ni pamoja na mashine za kuchakata korosho, mashine za kukaushia korosho, kumenya, meza za kusagia, umeme, maji pamoja na gharama nyingine.

"Mjasiriamali atahitaji kuwa na Sh. milioni 16.92 ambazo zitakuwa sawa na asilimia 20 tu ya jumla ya kiasi cha Sh. milioni 84.6 zinazohitajika kuendesha kiwanda cha kubangua korosho."

Alisema kiasi kinachobaki cha Sh. milioni 67.68 ambacho ni sawa na asimilia 80 ya mahitaji kitapatikana kwa kupitia mkopo kutoka benki itakayoshirikiana na kampuni hiyo kudhamini mradi.

"Kwa hesabu za haraka haraka, kila mjasiriamali ataweza kupata faida ya Sh. milioni 37.8 kwa mwaka baada ya kutoa gharama zote za uzalishaji," alisema.

Gupta alisema baada ya kumaliza kulipa mkopo kwa muda wa miaka mitatu, kiwanda cha kubangua korosho kitabaki kuwa ni mali ya mjasiriamali.

Alifafanua kuwa Tanzania itaokoa hadi Dola za Kimarekani milioni 300 kwa mwaka kutokana na kuongeza thamani ya korosho ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikiuzwa nje ya nchi bila kuongezwa thamani. Alisema katika awamu ya kwanza ya miaka mitano, mradi utasaidia kubangua tani 15,000 za korosho ya Tanzania kwa mwaka.

Alisema ndani ya miaka 15, wamelenga kuhakikisha korosho yote inayolimwa Tanzania inabanguliwa nchini ili kutengeneza ajira zaidi kwa wazawa.

Alisema kwa sasa, zaidi ya asilimia 90 ya korosho inayozalishwa nchini huuzwa bila kubanguliwa.

# TPA yajipanga kuongoza Afrika kwa shehena

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imesema maboresho makubwa wanayoendelea kuyafanya yataiwezesha kuongoza kwa kuwa bandari kubwa inayopokea magari mengi Afrika Mashariki hadi Kusini mwa Afrika.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Deusdedit Kakoko, wakati akizungumza na wahariri na waandishi waliotembelea Bandari ya Dar es Salaam.

Alisema kwa mwaka 2016/2017 walikuwa wakipokea magari 47,000 na sasa wana uwezo wa kupokea na kuhudumia magari 170,000 na magati yanayoendelea kujengwa yatawawezesha kupokea hadi 200,000.

Alisema gati namba moja hadi nne ambayo yamekuwa yakitumika, yamewasaidia kupokea meli kubwa za bahari kuu za kimataifa tofauti na ilivyokuwa kabla ya ujenzi.

Alisema takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa meli kubwa za bahari kuu zinapungua kwa idadi, lakini zinaongezeka kwa ukubwa na uwezo tofauti na ndogo zilizokuwa zinakuja kwa wingi.

"Tafsiri yake ni kwamba sasa hivi tunapokea meli kubwa na za moja kwa moja badala ya kuachiwa na jirani zetu wa kaskazini na wale wa kusini na tunashusha magari 1,000 hadi 2,000 kwa wakati mmoja kutoka magari 500 tuliyokuwa tukishusha zamani," alisema Kakoko.

Alisema kwa upande wa shehena kama nafaka na saruji, wanapokea meli kubwa kwa kuwa miaka minne iliyopita walikuwa wakipokea zenye urefu wa mita 230 na walipopokea yenye urefu wa mita 261 waliona kama miujiza.

Alisema ingawa wakati huo walifurahia kupokea meli zenye urefu wa mita 261, lakini kwa sasa zimekuwa za kawaida kutokana na maboresho waliyoyafanya wanapokea meli zenye urefu wa mita 280 na zaidi.

Kuhusu shehena ya kontena, Kakoko alisema walikuwa wakishusha kontena 500, lakini sasa hivi ni kawaida kushusha shehena ya kontena zaidi ya 1,500 kwenye bandari hiyo na wanatarajia idadi hiyo kuongezeka mara dufu baada ya ukarabati.

# Waliokopa mabilioni ya pembejeo wachunguzwa

**Ndalike Sonda,** BARIADI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Simiyu imeanza uchunguzi kubaini jinai kwa wakopaji 10 waliokopa Sh. bilioni 102 kupitia Mfuko wa Pembejeo Tanzania (AGITF).

Fedha hizo zilikopwa mwaka 2006, lakini mpaka leo hawajazirejesha kwenye mfuko.

Akizungumza na waandishi wa habari, mjini Bariadi Mkuu wa TAKUKURU, Mkoa wa Simiyu, Joshua Msuya, alisema kiasi hicho cha fedha mpaka sasa hakijarejeshwa na wakopaji hao licha ya kurejesha kwa wakati.

Alisema wakopaji hao kati yao, sita wanatoka katika Wilaya ya Bariadi ambao wanadaiwa zaidi ya Sh. milioni 500, Meatu mkopaji mmoja anadaiwa Sh. milioni 34, Maswa wapo wakopaji wawili ambao wanadaiwa Sh. milioni 413.8 na Busega mkopaji ni mmoja anadaiwa Sh. milioni 653.

Msuya alisema licha ya lengo jema la mikopo hiyo kuwanufaisha wakulima kupitia sekta ya kilimo kwa kuwakopesha zana za kilimo, zikiwamo trekta bado baadhi yao wamekuwa na utata kufanya marejesho licha ya jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na mfuko huo.

"Tunaendelea kuchunguza katika kipindi hiki cha robo ya kwanza ya mwaka, tumeendelea kufanya ufuatiliaji na uchunguzi na tumewaelekeza wahusika wa mikopo kufanya marejesho ili kufikia malengo ya mfuko huo kuwanufaisha wakulima kwani kama unakopa na unarejesha ni wazi kwamba unatoa fursa na wengine kuchukua mikopo hiyo," alisema Msuya.




Wananchi wa Kata ya Nyasubiasi, wakiangali basi la kampuni ya Kisbo Safari lenye namba za usajili T.231 DST, likiwa limeanguka wakati dereva wake alipokuwa akijaribu kumkwepa bibi kizee aliyekuwa akivuka barabara ya Isaka, wakati likitokea kituo kikuu cha mabasi mjini Kahama, mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: SHABAN NJIA** .

## Basi laua, 44 wanusurika

**Na Mohab Dominick, KAHAMA**

MTU mmoja amefariki dunia, huku 44 wakinusurika katika ajali ya basi la Kampuni ya Kisbo Safari ambalo lilikuwa linatoka wilayani Kahama, mkoani Shinyanga kuelekea jijini Dar es Salaam juzi alfajiri. Ajali hiyo ilitokea majira ya asubuhi saa 12.

Akizungumza na Nipashe eneo la tukio, shuhuda wa ajali hiyo, Elias Jeremia, alisema chanzo ni bibi aliyekuwa katikati ya barabara ya Isaka tokea stendi kuu ya mabasi.

Bibi huyo ambaye jina lake wala umri wake havikufahamika aligongwa na kupoteza maisha hapo hapo.

"Mbele ya basi la Kisbo kulikuwa na basi lingine ambalo mimi nilikuwa nimelipanda, lilimkwepa bibi huyo na mimi nilikwenda kushuka mbele, wakati wa kurundi tu nikaona basi la Kisbo nalo linamkwepa na kuanguka," alisema Jeremia.

Dereva wa basi hilo, Raraja Abdullah, alisema: "Basi langu lilikuwa na abiria 44 wakati natoka stendi kuu ya mabasi tuliondoka salama, lakini tulipofika eneo la Nyasumbi Msikitini alitokea bibi kwenye barabara katikati, nilivyomwona nilijaribu kumkwepa ndipo basi likwenda kutumbukia kwenye mfereji wa maji."

Alisema kwa kuwa hapakuwapo na majeruhi, kampuni ilitoa basi lingine na abiria kuendelea na safari kuelekea jijini Dar es Salaam.

Jeshi la Polisi limethibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema chanzo cha ajali ni bibi ambaye alikuwa katikati ya barabara akitembea, ambapo dereva wa basi hilo alijaribu kumkwepa bibi hiyo ndipo basi hilo lilikwenda kwenye mtaro wa maji.

## BAKITA yasisitiza fursa za Kiswahili

**Na Christina Mwakangale**

WATANZANIA wameshauriwa kukitumia Kiswahili kama bidhaa ili kujipatia kipato kutokana na kasi ya kukua kwake.

Mhariri Mwandamizi wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Onni Sigalla, alisema hayo alipokuwa akizungumza kituo kimoja cha redio kuhusu maadhimisho ya lugha hiyo yaliyoanza jijini Dodoma.

Alisema lugha ya Kiswahili inaendelea kuwa fursa hivyo watumiaji ikiwamo wazungumzaji, wakalimani, wafasiri na walimu, waitumie ipasavyo.

"Kiswahili kinazungumzwa na takribani watu milioni 100. Kiswahili ni bidhaa kwa maana inauzika kwa maana ya kufundishia, kukiandika na ni utamaduni," alisema Sigalla.

Kadhalika, alisema Watanzania wawe watumiaji wa bidhaa hiyo kwa kununua machapisho, vitabu vilivyoandikwa kwa Kiswahili ili kukuza mapato ya ndani.

"Ukinunua kitabu kutoka lugha nyingine umeongeza mapato kwa wengine, kubidhaisha lugha wakati mwingine si kuzungumza tu, kuna lugha ya alama pia," alisema Sigalla.

## Tigo yazindua huduma ya 'Lipa Kwa Simu'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo Tanzania, imezindua tena huduma ya malipo.

Huduma hiyo ya malipo awali ilitambulishwa mwaka 2014 kwa jina la 'Lipa Hapa kwa Tigo Pesa' ili kuwafanya wateja kununua bidhaa mbalimbali kwa njia ya kidijitali.

Kwa sasa huduma hiyo imepewa jina la 'Lipa kwa Simu', ambapo imekuja ikiwa imeboreshwa zaidi na kwamba mteja atatumia kufanya malipo mbalimbali bila kutumia namba za QR na zingine katika kupata huduma.

'Lipa kwa Simu' ni huduma ya kifedha ya kidijitali inayomfanya mfanyabiashara au taasisi kupokea fedha kutoka wateja wanaotumia simu za mkononi.

Akizungumza katika uzinduzi huo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Fedha cha Tigopesa, Angelica Pesha, alisema: "Soko la ndani lina sifa ya ukuaji mkubwa kwa idadi ya watu, idadi ya vijana na viwango vya juu vya data na kupitishwa kwa njia ya kidijitali.

"Madhumuni yetu ni kutanua na kuboresha njia zote za malipo nchini Tanzania. Tunaamini, huduma mpya ya Lipa kwa Simu, itawapa wateja wote wa Tigopesa pamoja na watumiaji wengine wa pesa, uzoefu mkubwa wa malipo kwa kuwawezesha kufanya shughuli zao zote za malipo kwa njia salama na rahisi."

"Pamoja na kuletwa kwa namba za QR na namba zingine katika Lipa kwa Simu tumejipanga kuleta ubunifu na usanifu kwa shughuli za Tigopesa.

"Kwa wafanyabiashara, tunaanzisha uzoefu wa ndani ya programu ambapo wataweza kusimamia ushuru wao wa malipo kupitia App ya Tigopesa, hii itaruhusu urahisi na udhibiti zaidi wa fedha za biashara," alisema.

Uzinduzi huu pia unaenda sambamba na promosheni ambayo itakuwa ni kwa ajili ya wateja wote wakipata ongezeko la fedha kila watakapotumia huduma ya 'Lipa Kwa Simu'.

Alisema huduma hiyo itakuwa inapatikana katika maeneo mbalimbali ikiwamo sokoni, sheli za mafuta, cinema, sehemu za vyakula, hotelini, wanapouza vinywaji, supermarket, maduka ya dawa na wanapouza vifaa vya ujenzi.

Alisema huduma hiyo itatumia kwa wateja wote wa Tigopesa na haina haja ya kujisajili.

# TAKUKURU yaokoa fedha za ujenzi wa zahanati

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Pwani, imeokoa Sh. 4,086,000 katika Wilaya ya Kisarawe, zikiwamo fedha zilizochangwa na wananchi kwa ajili ya ujenzi wa zahanati.

Akizungumza na waandishi wa habari Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Sadiki Nombo, alisema Sh.1,400,000 ambazo ni sehemu ya Sh. 2,175,000 zilizochangwa na wananchi wa Kijiji cha Marui Gwata kwa ajili ya ujenzi wa zahanati.

Nombo alisema fedha hizo zilifujwa na aliyekuwa mwenyekiti wa kamati ya ukusanyaji fedha za kijiji hicho, Jumanne Bilo.

Inadaiwa mtuhumiwa baada ya kukusanya michango hiyo hakuwasilisha kijijini kama inavyotakiwa, ndipo TAKUKURU ilipoingilia kati na kuanza uchunguzi.

Nombo alisema taasisi hiyo imesimamia suala hilo kuhakikisha mtuhumiwa anarejesha fedha hizo kwa matumizi yaliyotakiwa, ya kiasi kilichosalia Sh. 775,000 mtuhumiwa ameahidi kurudisha mwezi huu.

Aidha, alisema katika Shule ya Sekondari ya Kimani, aliyekuwa mkuu wa shule alifanya ubadhirifu wa Sh. 626,000 zikiwa fedha za ujenzi wa shule na kuwa TAKUKURU inasimamia suala hilo na mtuhumiwa ameahidi kurejesha ndani ya miezi miwili.

Wakati huo huo, Nombo alibainisha kuwa kiasi cha Sh. 2,060,000 sehemu ya Sh. 7,980,000 fedha za malipo ya nauli ya walimu wa shule za msingi zilizofanyiwa ubadhirifu na watumishi wa idara ya uhasibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

Hata hivyo, Nombo alisema watuhumiwa wameahidi kuendelea kurejesha fedha hizo.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara inayounganisha eneo la Kimara na Goba, jijini Dar es Salaam jana, kwa kiwango cha changarawe. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Serikali yaifagilia sheria ya udhibiti wa kemikali

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

SERIKALI imesema sheria ya usimamizi na udhibiti wa kemikali viwandani na majumbani ya mwaka 2003 imesaidia kujua aina ya kemikali zinazoingizwa nchini na matumizi yake.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Mwanza na Ofisa Biashara Mkoa wa Mwanza, Yesaya Sikinde, katika mafunzo ya usimamizi wa shughuli za kemikali, kanda ya ziwa iliyowahusisha wataalamu 80 wa masuala ya usimamizi wa kemikali.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Tutuba, Sikinde alisema ili kudhibiti madhara yanayosababishwa na matumizi ya kemikali yasiyo salama, serikali ilitunga sheria hiyo na kabla ya kutungwa na utekelezaji wake kuanza bidhaa hizo zilikuwa zikiingizwa nchini na kutumika pasipo usimamizi na udhibiti.

Miongoni mwa kemikali zilizokuwa zinaingizwa na matumizi yake kutofuatiliwa ni pamoja na tindikali na zebaki.

Hata hivyo, baada ya sheria hiyo kupitishwa kumekuwa na usimamizi na udhibiti wa kemikali kuanzia uingizaji, usafirishaji, utumiaji.

Alisema mpaka sasa wafanyabiashara 2065 na maghala yaliyochaguliwa kwa mwaka 2019 hadi 2020 yakiwa 1,672 , udhibiti huo umewezesha serikali kutambua mapema aina za kemikali zinazoingia nchini, mahali zinapokwenda na matumizi yake hivyo kupunguza madhara yake kwa wananchi na mazingira.

"Athari za matumizi mabaya yanaweza kusababisha magonjwa kwa binadamu yakiwamo saratani, mfumo wa uzazi, urithi, upumuaji na hatimaye kifo pamoja na kuathiri mazingira kama maji, misitu na kudhuru wanyamapori.

Mratibu wa ukaguzi wa serikali kwa niaba ya Mkurugenzi wa Idara ya Uthibiti Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Magdalena Mtenga, alisema wanafanya mafunzo hayo ya siku mbili ili kuwajengea uwezo katika masuala ya udhibiti na usimamizi wa kemikali.

## Kasi yatakiwa mchakato umilikishaji wa hifadhi

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imetakiwa kuharakisha mchakato wa kumilikisha kisheria taasisi yenye uwezo eneo la Hifadhi ya Manyamapori ya Isawima wilayani Kaliua ili kukomesha uharibifu maliasili unaofanyika katika eneo hilo.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philimen Sengati, wakati wa ziara yake ya kukagua shehena ya magogo yaliyokamatwa katika visiwa mbalimbali vilivyomo katika msitu huo, baada ya wavunaji haramu kutoroka.

Alisema kukosekana kwa taasisi yenye mamlaka ya kisheria ya kuusimamia imepelekea uharibifu katika Hifadhi ya Manyamapori ya Isawima wilayani Kaliua kuwa kubwa.

Dk. Sengati alisema hata Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Isawima haijakabidhiwa kisheria kwa sababu haijakamilisha hatua zote zinatakiwa kuiwezesha kusimamia kikamilifu, hivyo kushindwa kuwa na nguvu za kudhibiti uharibifu ndani yake.

Alisema hali hiyo imesababisha Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Wakala wa Mistu Tanzania (TFS) kukaa pembeni kwa sababu taasisi hizo na Jumuiya ya Isawima hawana nguvu za kisheria kusimamia msitu huo.

Dk. Sengati alisema ni vema mchakato uliokuwa umeanza wa kutaka msitu huo uwe na chombo kimoja kinachousimamia kisheria ukaendelea na kumalizika kwa ajili ya kuwa na msimamizi atakayeweza kudhibiti wavunaji haramu wa miti ya asili.

Mkuu huyo wa Mkoa alisema kasi ya uvunaji haramu wa magogo inatisha na kuongeza kuwa hatua za haraka zisipochukuliwa kudhibiti uharibifu ndani ya msitu huo ndani ya muda mfupi.

ama
ALHAMISI JANUARI 21, 2021
AFYA NA MAZINGIRA





Ukurasa 14

Mazingira ya Jiji Dar yanavyolindwa na wanaouza miche ndani ya mitaa



Ukurasa 13

**Nyama iliyosheheni mashabiki wengi, daktari akiwapa 'vigezo na masharti'**

# Corona ilivyopaisha matumizi ya tiba asili kwa wahitaji Tanzania

- Mti wa mkaratusi, malimao vyang'ara
- Serikali: Wahitaji tiba hiyo ni wengi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TANZANIA imebarikiwa miti mingi ambayo ni tiba ya magonjwa mbalimbali. Hilo limethibitika wakati wa janga la corona, watu wengi kutumia mitishamba ambayo iliwapa ahueni kubwa na kupona kabisa.

Mimea mingi ilithibitika kusaidia watu wengi wenye matatizo mbalimbali ya mfumo wa hewa kama kifua, homa, mafua na magonjwa mengine.

Hapo inajumuisha matawi ya mwarobaini, mvumbasi, mchaichai, mpera, malimao, mkaratusi, tangawizi na mimea mbalimbali ya kujifukiza, ili kuondoa kirusi hicho mwilini.

Dawa hizo za asili hutumika ama kwa kujifukiza au kunywa. Hapo inabeba maana ya kuchemsha aina mbalimbali za mimea, kisha mgonjwa anakaa kwenye kigoda na kufunikwa shuka ili kupata mvuke anaouvuta, akiwa amefunikwa na kuingia moja kwa moja kwenye mfumo wake wa upumuaji.



Muuzaji malimao, Harun Iddi katika Soko la Majengo, Dodoma, bidhaa iliyoongezeka sokoni, kutokana na kutumika kutibu corona. **PICHA: MTANDAO**

Majani ya mkaratusi yamekuwa yakitumika kama tiba kwa watu kujifukiza. Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Tiba Asili na Tiba Mbadala Mkoa wa Dodoma, Mohamed Mdoe, anathibitisha hilo.

Hiyo ni baada ya ugonjwa huo kuibuka nchini na wananchi kutumia dawa mbalimbali za kujifukiza, huku kukikosekana mti maalum au dawa, isipokuwa mkaratusi unaonekana kutumiwa na wengi.

"Mti uliotumika kwa kiasi kikubwa ni mkaratusi waliupenda sana na kwa sababu huu mti ni mzuri hasa kwa maradhi mbalimbali, wazee wa zamani walikuwa wanapenda kutumia dawa hii.

"Kwa hiyo, tukachukulia wazee wetu wa zamani kama vile kipindi cha ugonjwa wa ndui watu walikuwa wakiogeshwa mti huo kuna maradhi kama UTI (maambukizi kwa njia ya mkojo na huathiri mfumo wa mkojo), mtu anachemshiwa huo mti anakunywa," anasema.

Anasema majani ya mti huo yalitumiwa na watu wengi kutokana na sifa za kutibu maradhi mbalimbali kwenye mwili wa binadamu.

Mdoe anasema, kila mwananchi alikuwa na namna yake ya kutafuta mti huo ambao kwa Dodoma si mingi, ikilinganishwa na mikoa ya Tanga na Kilimanjaro.

Anafafanua kwamba kuna wakati watu wa Dodoma walikuwa wanaagizia mkoani Tanga ili kupata majani hayo ya mkaratusi.

"Kukata matawi kila mmoja alikuwa nakwenda kivyake hapakuwapo na kubebana kwa pamoja kwenda kukata na kila mmoja alikuwa anajua anapata eneo gani mti huu, tunashukuru hali ni nzuri kwa sasa," alisema.

Anaongeza: "Wakati wa corona kila mmoja alikuwa anaangalia njia gani kikwao au kikabila, hivyo walikuwa wanaangalia ni dawa gani inayofaa siyo dawa maalum kwa corona, kila mtu alitumia dawa kulingana na anavyoamini kikwao."

Anabainisha matumizi hayo ya tiba mbadala kwa kujifukiza ilisaidia watu wengi kufanikiwa hasa waliokuwa wakihisi mafua au homa inayofanana na dalili za ugonjwa huo.

Mdoe anasema: "Kila mmoja alitafuta namna ya kujinusuru hakukuwa na dawa maalum ya kutumia kwa ajili ya corona, wazee walitufundisha matumizi ya dawa hizi, sisi kama wataalamu wa tiba.

"Tulikuwa tunafuatilia watu walikuwa wanaomba ushauri wa dawa hasa za kujifukiza, tulikuwa tunawaelekeza watumie mti fulani, mwamko ulikuwa mkubwa."

Mwenyekiti huyo anaeleza kuwa walikuwa wakiwapa ushauri wa dawa hizo kuchemsha na kujifukiza na siyo za kunywa. Anafafanua:

"Watu walikuwa wakienda porini huko kutafuta na kuwauzia watu, wengine kusaidiana bure hakukuwa na gharama maalum, kila mtu alikuwa na namna yake, walikuwa wanapeana tu, ni mtu kuelekeza tumia dawa hii au hii."

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Corona ilivyopaisha matumizi ya tiba asili kwa wahitaji Tanzania

INATOKA UK.11

**TAARIFA YA NIMR**

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu, Prof. Yunus Mgaya, wakati wa corona nchini, alisema ikiwa watu watatumia mimea zaidi ya minne, upo uwezekano wa dawa hizo kuanza kupambana zenyewe katika utendaji badala ya kumsaidia mgonjwa.

Anaifafanua mchanganyiko unaotakiwa, kundi la kwanza ni mchanganyiko wa majani ya mkaratusi, majani ya kivumbasi (kashwagala) na mchaichai; kundi la pili ni mchanganyiko wa mchaichai, karafuu, tangawizi iliyopondwa na majani ya limao; lingine ni majani ya mwarobaini, majani ya mpera, mchaichai na majani ya mlimao.

Prof. Mgaya anasema mtu anatakiwa kutumia gramu 50 za majani ya mkaratusi, gramu 50 za kivumbasi na gramu 20 za mchaichai na kwamba tiba joto hiyo au mvuke ni muhimu kusaidia kuongeza kinga ya mwili, kufungua njia ya hewa na kurarua virusi vya corona, kama bado vimo kwenye njia ya hewa na havijaingia kwenye mapafu.

**MASHUHUDA WATUMIAJI**

Mtumiaji dawa hizo, Edward Mathias, anasema alihisi dalili za ugonjwa h akiwa nyumbani na akaamua kujitenga kwa wiki nzima, huku akijifukiza kwa kutumia mimea minne ikiwamo, mkaratusi, mvumbasi, mchaichai na tangawizi.

Anasema kwa muda mfupi hali hiyo ya kuumwa mwili na mafua yasiyopona iliondoka na hadi sasa hajasikia hali ya aina hiyo mwilini mwake. Mtahias anasimulia:

"Miajani ya mkaratusi niliyapata kwa jirani yangu, mvumbasi unapenda kuota kwenye viwanja vya mpira, nikapata mimea yote minne nilikuwa nachemsha maji kwanza yakichemka ndio natumbukiza majani haya.

"Kwa dakika chache tu nikiwa nimefunikia, baada ya hapo nasogeza jiko likiwa limebandikwa sufuria najifunika shuka kwa ajili ya kujifukiza.

"Yaani ule mvuke nausikia kabisa unaingia kwenye mfumo wa hewa. Nilikuwa natumia dakika 10 kukaa humo kila siku jioni, nikitoka naoga maji ya vuguvugu ili kuondoa kirusi maana wataalamu walituambia kirusi kina asili ya mafuta, kweli kufukiza kumenisaidia."

Mnamo Mei 17 mwaka jana, Rais John Magufuli akitoa salamu kwa Watanzania aliposhiriki ibada ya Jumapili akiwa Chato mkoani Geita, aliwaambia kuwa mtoto wake aliambukizwa virusi vya corona, lakini alipona baada ya kujitenga, kunywa malimao na kujifukiza.



Mwakilishi wa Kikundi cha Shekilindi Bonsnia Ant Covid mjini Dodoma, Bashiru Iddy, akionyesha chupa ya dawa iliyotumiwa na wananchi wakati ugonjwa wa corona, ulipokuwapo nchini. **PICHA: MTANDAO**

> **Kwa dakika chache tu nikiwa nimefunikia, baada ya hapo nasogeza jiko likiwa limebandikwa sufuria najifunika shuka kwa ajili ya kujifukiza.**

**WATENGENEZA DAWA**

Mapema mwaka jana, Mkurugenzi wa Kitengo cha Tiba Asili kutoka NIMR, Dk. Justine Omolo, alisema dawa ya NIMRCAF iliyofanyiwa utafiti na taasisi hiyo, ilionyesha matumaini ya kudhibiti ugonjwa huo.

Dk. Omolo anasema dawa hiyo ni kanuni ya tiba lishe yenye mchanganyiko wa pilipili kichaa, tangawizi, limao, kitunguu saumu, asali na maji na inasaidia kumpa nafuu mgonjwa wa corona, kwa kudhibiti dalili zake.

"Mchanganyiko wa tiba lishe hiyo sio dawa ya corona, lakini inasaidia kumpa nafuu mgonjwa kwa kuwa inatibu dalili zinazoambatana na ugonjwa huo, hadi sasa tiba lishe hii imeshaleta matokeo chanya kwa kuwa imesaidia wagonjwa wengi wa corona," anasema.

**WADAU WA DODOMA**

Mwakilishi wa Shekilindi Bosnia Ant Covid (dawa ya kutibu dalili za Corona), Dodoma, Bashiru Iddy, anasema usajili wa dawa hiyo umekamilika na Mkemia Mkuu wa Serikali amethibitisha kwamba haina sumukuvu yoyote na salama kwa matumizi ya binadamu. Hata hivyo hakuweka wazi mchanganyiko wa dawa alizotumia.

"Kipindi cha corona dawa hii imesaidia watu. Usajili wake upo vizuri, tumepata pia kibali kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na nyaraka zipo. Dawa inafanya kazi kwa kiasi kikubwa magonjwa ya kifua," anasema.

Bashiru anasema wakati wa corona, chupa ya dawa anayouza ilikuwa Sh. 30,000 na mtu mwenye dalili za ugonjwa huo alishauriwa kunywa chupa hiyo, pamoja na glasi tatu za juisi ya miwa.

"Baada ya saa nne alikuwa anatakiwa kunywa chupa ya pili, pia baada ya saa nne anakunywa chupa ya tatu. Hivyo, mtu mwenye dalili hizo alikuwa anapata tiba.

"Dawa hii imetengenezwa na aina tatu za miti ambayo kitaalamu hatuwezi kuweka wazi ili wengine wasije kufanya utapeli utakaosababisha madhara kwa jamii," anasema.

**WAUZA DAWA ASILI**

Muuza dawa asili, Josephina Peter, anasema mwitikio wa watu kujifukiza wakati wa corona ulikuwa mkubwa na wananchi walinunua mkaratusi, mvumbasi na mwarobaini.

Muuzaji wa dawa za tiba asilia, Mariamu Masudi, anasema awali mimea au dawa hizo zilijulikana kwa matumizi mengine, lakini kutokana na ugonjwa huo zilitumika kujifukiza ili kuondoa kirusi hicho mwilini.

**MATUMIZI YA MALIMAO**

Mfanyabiashara katika Soko Kuu la Majengo jijini Dodoma, Harun Iddy, anasema wakati wa mlipuko wa corona nchini, bidhaa kama malimao, tangawizi na vitunguu saumu viliongezeka sana mahitaji yake sokoni.

Anatumia mifano akitumia vilelezo visivyo rasmi, kwamba kutokana na matumizi ya tiba mbadala, mfanyabiashara aliuza mifuko ya kilo 100, zaidi ya 500 kila siku.

Iddy anasema pamoja na mahitaji hayo makubwa, bidhaa hizo zilipatikana kwa wingi kuhudumia wananchi waliotumia kuchemsha na kijifukiza.

Anasema katikia kipindi cha mvua, malimao yalikuwa adimu na akalazimika kuzifuata nchi jirani Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Uganda na Sudan.

"Hii imetokana na mvua kunyesha kwa wingi nchini mwaka jana msimu wa pili wa malimao, haukuwapo hali ambayo imesabaisha bidhaa hiyo kuwa adimu," anasema.

Pia anasema kipindi hicho walikuwa wakiuzia mfuko moja wa kilo 100 kwa zaidi ya Sh. 250,000 na upatikanaji wake ulikuwa wa shida, wakati awali ilichukuliwa kama kitu cha kawaida.

"Zamani mtu ukimwambia unafanya biashara ya malimao anashangaa, lakini hivi sasa hata ukipita barabarani umebeba mzingo wa malimao watu wanakuulizia bei tofauti na zamani," anasema.

Mfanyabiashara Hassan Chitembedya, anasema malimao hivio sasa sokoni hayakai, kutoka na mahitaji makubwa na mengi yanasafirishwa nje ya nchi, ikiwamo Kenya kwa ajili ya matumizi ya tiba mbadala corona.

Kitaalamu, limao ingawa si tunda lenye virutubisho vingi vya vitamini C, lakini ni bora kwa kuwa na kemikali inayosaidia kutibu mafua na mfumo wa kupumua.

Maji ya limao yanatajwa kuwa na takriban miligramu 18.6 za vitamini C na vipimo kamili vya kila siku vinavyopendekezwa kwa watu wazima ni kati ya miligramu 65 na 90.

**WIZARA YA AFYA**

Mkurugenzi Msaidizi wa Tiba Asili na Tiba Mbadala wa Wizara ya Afya, Dk. Paulo Mhame, anakiri ujio wa ugonjwa huo nchini umesaidia huduma za tiba asili nchini kukubalika kwa wengi, pasipo kujali kiwango chao cha elimu na hadhi yao kijamii, mtazamo ulliokuwapo awali.

"Wengi wametumia kunywa hususani matumizi ya tangawizi, limao, vitunguu na vitunguu swaumu, pia katika kujifukiza kumewapaisha Watanzania ugonjwa wenyewe uklionekana sio kitu.

"Llakini hadi leo watu wanaendelea kujifukiza hata kama hawavai barakoa wala kunawa mikono na wanatumia mafuta tete kwa ajili ya kufukiza hususan matumizi ya kivumbasi, mchaichai na mkaratusi nao unatumika kwa wingi," anasema.

Anasema dhana ya kuona tiba asili ni ushiriki inaondoka, lakini kiserikali bado kuna kazi ya kuendelea kuelimisha wananchi matumizi ya huduma za tiba asili.

Mwaka juzi, dunia ilikumbwa na homa kali ya mapafu, inayosababishwa na virusi vya corona na kuripotiwa kwa mara ya kwanza mjini Wuhan, China na baadaye

INAENDELEA UK.14

AFYA

KITIMOTO

# Nyama iliyosheheni mashabiki wengi, daktari akiwapa vigezo

**Na Sabato Kasika**

• Unataka kula? Zingatia mambo haya hapa



Nyama ya nguruwe ikiwa buchani. **PICHA ZOTE: MTANADAO**

NYAMA ya nguruwe katika zama za karibuni, imeingia katika orodha ya kupendwa sana katika sura ya kitaifa.

Kihistoria nchini ilijulikana baadhi ya mikoa kama Mbeya kulikofugwa na kuliwa kwa wingi, lakini kadri muda ulivyoenda, hasa kuanzia mwishoni mwa miaka 1980, ulaji uliongezeka, Dar es Salaam, ikiibuka mwenyeji.

Leo imefikia hadhi kuwa miongoni mwa mlo unaopendwa sana mijini, ambako si haba imejaa kwenye bucha na mishikaki yake imejaa kwenye 'vituo vya msaada' vingi, vinavyojumuisha baa, baadhi ya wateja wakiunganisha na mseto 'moja moto moja baridi.'

Umaarufu wa nyama hiyo, umesababisha ipatiwe majina mengi bandia, ikiwamo 'Noah' na 'Kitimoto', ambayo sasa ina hadhi ya msamiati pori, ikiwa rasmi kila kona.

**SHIDA ILIYOPO**

Ulaji nyama hiyo inayowakonga walaji, pia ina upungufu wa kuzaa matatizo ya kuwa na magonjwa inajumuisha 'African Swine Fever' ambao ni minyoo ya tegu.

Ni aina ya maradhi yanayotajwa na wataalamu wa magonjwa ya mifugo kuwa mlaji nyama ya nguruwe anaweza kudhurika, iwapo itapikwa na kuliwa bila kuiva vizuri.

Utaratibu wa kitabibu wa kiserikali ni kwamba, kila penye mlipuko wa ugonjwa tegi unapowakumba nguruwe, serikali hupiga marufuku ulaji, uuzaji nyama yake hadi hali inapokuwa shwari, ndipo unaendelea.

Mtaalamu na mstaafu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Sero Hassan Luwongo, anaueleza kuwa ni ugonjwa usiokuwa na chanjo wala tiba, bali nguruwe kuwekwa ndani ya karantini hadi uishe.

Katika mazungumzo yake na Nipashe, Dk. Luwongo anasema, ulaji wa nyama ya nguruwe isiyoiva vizuri, inamsababishia mlaji kukumbwa na ugonjwa wa kifafa.

Anafafanua kuwa nyama ya nguruwe inapokuwa na minyoo na haijaiva vizuri, inasababishia mlaji kupata uvimbe kwenye ubongo na ndipo inafuata uwezekano wa kupata kifafa.

Dk. Luwongo anasema uvimbe wa ubongo upo wa aina nyingi, akiufafanua: "Nguruwe ana magonjwa kama walivyo wanyama wengine ambayo yanatibika, yakiwamo ya kwato, lakini minyoo ya tegu inayoitwa African Swine Fever, haitibiki na ndiyo yenye madhara."

Anasema, nyama ya nguruwe ina minyoo ambayo ni wagumu kufa, hali inayotoa uwezekano wakaingia mwilini na kujenga uwezekano wa kufika kwenye ubongo, jambo linalojenga uwezekano wa madhara hayo.

"Virusi hivyo havina tiba wala chanjo. Njia pekee ni kupika nyama na kuhakikisha imeiva vizuri, pia ugonjwa unapolipuka, ni kupiga marufuku usafirishaji, ulaji wa nyama ili kuzuia ugonjwa usisambae,|" anasema.

> **Virusi hivyo havina tiba wala chanjo. Njia pekee ni kupika nyama na kuhakikisha imeiva vizuri, pia ugonjwa unapolipuka, ni kupiga marufuku usafirishaji.**



Nyama ya nguruwe tayari kwa kuliwa.

**MLIPUKO NCHINI**

Ni ugonjwa unaotajwa kuibuka kila mara nchini na mwaka 2017 ulitua katika wilaya za Kalambo mkoani Rukwa na Dodoma na kusababisha viongozi kupiga marufuku ulaji nyama ya nguruwe.

Pia hatua ya karibuni ni kwamba umetua wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga, unadaiwa kuua nguruwe zaidi ya 500 na serikali kupitia ofisi ya wilaya, alipiga marufuku uuzaji, usafirishaji na ulaji wa nyama ya nguruwe kwa muda usiojulikana hadi hali itulie.

Mkuu wa Wilaya, Anamringi Macha, anasema ni hatua ya kudhibiti kuenea maambukizo ya ugonjwa huo unaodaiwa kuua nguruwe kwa kasi wilayani kwake na wataalamu wetu wanaendelea kufanya utafiti kuhakikisha wanaudhibiti, ili kuzuia madhara zaidi yasijitokeze.

Aidha, Macha anawataka walaji nyama ya nguruwe wilayani mwake kuachana nayo hadi watakapotangaziwa na serikali, hivyo watumie mbadala wa nyama ya mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku kwa kuwa hawajaathiriwa na ugonjwa huo.

**KULIVYO DUNIANI**

Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na The International Agency for Research on Cancer unamtaja nguruwe ni mnyama, nyama yake inaliwa kwa wastani na asilimia 38 ya wakazi wote duniani.

Hata hivyo, anatoa kasoro kuwa nyama hiyo ina madhara makubwa, akitaja ni sumu ya anayoiita 'carcinogen' inayosababisha ugonjwa wa saratani.

Kwa mujibu wa watafiti hao wa WHO, wanaainisha pale kila siku mtui alapo gramu 50 ya nyama ya nguruwe, ana uwezekano wa kupata saratani kwa watani wa asilimia 18. Utafiti uliofanyika 1998 wa WHO, ulionyesha nyama ya nguruwe iliyopikwa kwa nyuzi joto 104C, bado zaidi ya nusu (asilimia 52.37) ya minyoo iitwayo 'trichinella worm' hawafi.

Hiyo ni minyoo ambayo inapoingia mwilini mwa binadamu, husababisha ugonjwa uitwao 'trichinosis' ambao dalili zake kwa mgonjwa zanajuimuisha homa kali; kichwa kuuma; kukosa nguvu; maumivu ya nyama za mwili; macho kuwa rangi ya pinki; kuvimba uso na kope; na kudhuriwa na mwanga.

WHO inatahadharisha namna kuwapo minyoo aina tofauti waitwao kitaaalamu ' Taenia solium' mlaji nyama anaweza kuipata isipopikwa vizuri na inasababisha matatizo ya mfumo wa fahamu na ndio chanzo cha maradhi ya kifafa.

Pia inaelezwa ni aina ya nyama yenye virusi vinayosababisha homa ya ini aina 'E' na kuna kuna wadudu wanaobaki ambao nao wana madhara tofauti mwilini kwa binadamu mlaji.

.

**FAIDA NA HASARA**

Hadi sasa inaelezwa asilimia 30 ya wagonjwa wote duniani wenye kifafa huwa ni wanaoshambuliwa na minyoo hiyo ipatikanayo kwenye nyama ya nguruwe isiyoiva vizuri.

Inaelezwa kuwa watu milioni 50 duniani kote wenye kifafa ni walaji wa nyama ya nguruwe kwa namna tofauti kama vile soseji, au nyama iliyopikwa.

Pia kuna faida ikitajwa vitamini muhimu katika mwili wa binadamu; ambazo ni B1, B6 na B12 na walaji wanapata madini chuma, yanayowasaidia kuimarisha mifupa, huku magnesium inayosaidia mwilini mwa binadamu.

Mengine ya manufaa ni viini lishe vya protini ya kutosha, ambayo inachangia kujenga mwili, pia mafuta yanayoufanya mwili kupata nguvu.

Nyama ya nguruwe inaingia katika orodha ya kuimarisha ngozi ya mlaji kuifanya iwe laini.

MAZINGIRA

# Mazingira ya Jiji Dar yanavyolindwa na wanaouza miche ndani ya mitaa

• Kilio: Elimu ndogo, mauzo yanasuasua

**Na Maulid Mmbaga**

UPANDAJI wa miti ni harakati inayohimizwa katika mataifa yote duniani. Lengo kubwa ni kuhakikisha miti mingi zaidi inapandwa, ili kusaidia mabadiliko ya tabianchi.

Katika kulihimiza hilo, wapo wauzaji wa miche ya miti wanachangia kwa kiasi kikubwa katika utunzaji mazingira, ingawa kuna sura nyingine ya kutokuwapo mwitikio wa kutosha katika ununuzi wa miti hiyo.

Biashara ya uuzaji miche ya miti nchini, hususan katika Jiji la Dar es Salaam tayari ina miaka mingi, wauzaji bado wanalalamika kuwapo hali ya kusuasua.

Umoja wa Mataifa katika Ripoti ya Mwaka 2020, inawataka viongozi wa mataifa yote duniani, kulichukulia jambo la upandaji ni la dharura.

Ripoti hiyo ilieleza kwamba kutoka mwaka 1994 hadi 2020 zaidi ya hekta 420 za misitu zimepotea kutokana na watu kukata miti na kuweka miundombinu mbalimbali ikiwamo kujenga makazi, hivyo ni jukumu la kila mtu kuhakikisha anapanda mti hata mmoja katika mazingira anayo ishi.

Pia kunasisitizwa umuhimu wa kila mmoja, kufahamu kwamba uharibifu wa mazingira unasababisha umaskini, sambamba na madhara mbalimbali ya moja kwa moja.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, madhara yanayoangukia humo yanajumuisha shida ya upatikanaji majisafi, rutuba nzuri katika udongo, mazao na huduma nyingine muhimu za afya na maisha ya binadamu.

Aidha, katika umaskini, pia kunatajwa madhara ya uharibifu wa mazingira yanayoangukia katika kudhoofisha juhudi na uwezo wa binadamu kusimamia na kutumia rasilimali kwa njia endelevu.



Katibu Tarafa wa Mbagala wilayani Temeke, Bertha Minga, akiongoza kampeni ya Manispaa ya Temeke, kupanda miti iliyofanyika mwaka 2018. **PICHA: MTANDAO**

> **Nashauri watu wawe na utaratibu wa kupanda miti mingi katika mazingira yao, kwani ina faida nyingi, ikiwamo utunzaji mazingira.**

**SERA YA TAIFA**

Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997, inaainisha vikwazo sita vilivyoko ambavyo ni uharibifu wa ardhi; uharibifu wa misitu; kupotea kwa makazi ya viumbepori na baianuai; kukosekana maji salama mjini na vijijini; kupungua ubora wa mifumo ya maji; na uchafuzi wa mazingira hasa katika maeneo ya mijini.

Hizo zinatakwa kuingia katika orodha ya vikuu vinavyochangia kuzorotesha ukuaji uchumi na juhudi za serikali katika kupunguza umaskini, hivyo kuathiri maisha na ustawi wa jamii.

Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, inaeleza wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali kuanzia, serikali za mitaa hadi taifa.

Mambo yanayosisitizwa katika sheria hiyo yanajumuisha mazingira kupitia; mipango na usimamizi wa matumizi endelevu; kudhibiti uchafuzi wa mazingira; utunzaji taarifa na takwimu zake; utafiti na ushiriki wa jamii; utekelezaji wa majukumu yatokanayo na mikataba ya kimataifa.

Mengine yanayotajwa ni utii na utekelezaji wa sheria, pamoja na matumizi ya dhana mbalimbali za kusimamia hifadhi ya mazingira hususani tathmini ya athari katika mazingira; tathmini ya mazingira kimkakati; na dhana za kiuchumi na viwango vya mazingira.

Hadi sasa, tayari kuna kanuni, miongozo na programu mbalimbali zilizotungwa kufanikisha utekelezaji sheria hiyo na ni jukumu la serikali, wadau wa mazingira na wananchi kwa jumla kuhakikisha utunzaji mazingira unazingatiwa.

**WAUZA MITI**

Wauza miti wanasema, uhusiano kati ya miti na mazingira uko wazi, lakini kwa upande wao wanashuhudia aina ya sintofahamu katika mauzo, kutokana mwitikio mdogo wa wananchi katika kuunga mkono suala hilo.

Alli Ramadhani, mkazi wa Tabata Kinyerezi, Dar es Salaam, anasema katika biashara hiyo wapo baadhi ya watu wanaopenda mazingira na hao ndio mara nyingi wananunua miti ya kuipanda katika mazingira yao.

Anasema kati ya miti anayouza ni pamoja ni ya matunda na inayotumika kwa nafasi ya dawa, yote inabaki kuwa na faida inapopandwa katika mazingira ya nyumbani, inazalisha matunda na chanzo cha matibabu.

"Nashauri watu wawe na utaratibu wa kupanda miti mingi katika mazingira yao, kwani ina faida nyingi, ikiwamo utunzaji mazingira, kuleta kivuli nyumbani, pamoja na kusaidia kulinda ardhi," anasema Ramadhani.

Juma Simba, anayejihusisha na kuu miche ya miti, anasema katika biashara yake amejiwekea utaratibu maalumu wa kuwasaidia wateja kwa kuwapa elimu, namna ya kuipanda na kuitunza, mimea hiyo ikuwe vizuri. Muuza miche huyo anatoa wito kwa wadau wa mazingira na serikali, kuwatatulia changamoto ya upatikanaji vifungashio mbadala vinavyotumika kukuzia miche ya miti, kwani vina uhaba tangu kupigwe marufuku utumiaji mifuko ya plastiki.

Tabu Bakari, mkazi wa Dar es Salaam, ana maelezo kwamba suala la upandaji miti kwa wakazi wa jiji hilo, bado haridhii kiwango cha kipaumbele wanachokipa, kwani sababu ya mazingira yanayowazunguka hayaruhusu upandaji miti mikubwa.

"Asilimia kubwa ya wananchi tunamiliki maeneo madogo, hivyo si rahisi mtu kujiwa na wazo la kupanda miti mingi kutokana na uhaba wa eneo, 'sana sana' tunapanda maua kuyafanya mazingira yaonekane vizuri na miti midogo kwa ajili ya kivuli," anahitimisha Tabu.

## Corona ilivyopaisha matumizi ya tiba asili kwa wahitaji Tanzania

**INATOKA UK.12**

ukasambaa duniani.

Afya Duniani (WHO) kwa wagonjwa 56,000, ulibaini asilimia 80 ya walioambukizwa, hupata dalili zisizo kali kama vile kukohoa, joto mwilini na mara nyingine homa ya mapafu.

Pia asilimia 14 hupatwa na dalili kali kama vile tatizo la kupumua; asilimia sita wanakuwa na tatizo la mapafu kushindwa kufanya kazi na viungo vingine mwilini na hata kusababisha kifo.

Takwimu zinazotolewa kila siku na WHO, hadi kufikia Januari 6, 2020 wakati corona ilivamia dunia , kulikuwapo jumla wagonjwa milioni 83.32 na vifo 1,830,000 katika nchi zote zilizokumbwa.

Nchini Tanzania, mgonjwa wa kwanza aliripotiwa Machi 16, 2020 na serikali ilichukua hatua mbalimbali za kukabiliana nao, ikihimiza pia wananchi kutumia tiba ya asili jambo lililowasaidia kutojifungia (lockdown) na wengi waliendelea na shughuli zao.


Katika kipindi cha corona, Tanzania ilionekana kinara wa matumizi ya tiba hiyo, baada ya Rais John Magufuli kutoa wito kwa Watanzania kupitia hotuba zake mbalimbali kutumia ili kupambana na ugonjwa huo kwa kujifukiza, sambamba na ibada maalumu kupitia nyumba za ibada.

**SIMULIZI ZA WATUMIAJI**

Mkazi wa Dodoma, John Mnyahimbu, anasema majani hayo wakati wa kujifukiza yalimsaidia kutokwa na jasho kwa wingi na anayehisi mafua, mfumo wake wa hewa unafunguka.

"Mimi nilikuwa najifukiza mara moja kila siku jioni, nikirudi kwenye mihangaiko yangu. Nikifika na majani yangu nachemsha nimeyafunikia yakichemka napunguza moto halafu najifunika na nguo," anadokeza na kuendelea:

"Nakuwa nimeinamia ili kupata mvuke, nilikuwa naona inanisaidia hata viungo vya mwili vikionekana kuchoka ile ni kama sauna."





# Saratani mfuko wa kizazi yaongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SARATANI ya mlango wa kizazi, imetajwa kuongoza kundi la saratani zote za wanawake kwa Kanda ya Kati kwa asilimia 32, huku tezi dume ikiongoza kwa asilimia 39 kwa wanaume.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa idara ya magonjwa ya saratani, huduma za patholojia na mkataba wa mteja kwenye hospitali hiyo.

Dk. Chandika alisema kuanzishwa kwa daftari maalum la kuratibu maradhi ya saratani Kanda ya Kati mwaka 2018, saratani ya mlango wa kizazi ndio inaongoza kwa saratani zote zilizoratibiwa ikiwa na jumla ya wagonjwa 778 sawa na asilimia 32 ya saratani zote.

Alisema saratani ya tezi dume inaongoza kwa wanaume na wagonjwa 265 waliratibiwa sawa na asilimia 39.

Dk. Chandika aliongeza kuwa umri unaoathirika zaidi na maradhi hayo ni kati ya miaka 50 hasi 69 na jumla ya wagonjwa 1,089 sawa na asilimia 42.2 ya wagonjwa wote.

Awali, alisema takwimu za Shirika la IARC chini ya WHO zinaonyesha kwamba mwaka 2018 jumla ya watu 18.1 waligundulika kuwa na aina mbalimbali za saratani duniani, kati yao watu milioni 9.6 walifariki kutokana na magonjwa ya saratani.

# Jafo akerwa ufaulu mdogo Itega

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amekerwa na ufaulu mdogo katika Shule ya Sekondari Itega, jijini Dodoma, kwenye mtihani wa kidato cha nne uliofanyika mwaka jana, licha ya kuwa na walimu 40.

Akizungumza jana na walimu na wanafunzi wa shule hiyo, aliutaka uongozi kuhakikisha ufaulu unaongezeka kwenye mitihani ijayo.

Alimtaka Mkuu wa shule hiyo na Mwalimu wa Taaluma kuhakikisha inafanya vizuri kwa kuwa matokeo yake hayaridhishi.

"Hii shule ina walimu 40, lakini matokeo hayanifurahishi wala hayaniridhishi na haiwezekani wanafunzi watatu pekee ndio wamepata daraja la pili na daraja la tatu 18 huku alama ya zero zikiwa nyingi," alisema.

"Nimekuja hapa kuwataka mfanye bidii ili shule hii ya Sekondari Itega ifanye vizuri maana suala hili ni kama msiba kwenu na wazazi wenye wanafunzi matokeo sio mazuri hivyo badilikeni ili kimkoa mpande."

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo ameagiza kukarabatiwa kwa darasa la wanafunzi wa chekechea katika Shule ya Msingi Nkuhungu.

Alitoa wiki mbili kwa uongozi wa shule hiyo na Mkurugenzi wa Jiji kuhakikisha ifikapo Februari 22, mwaka huu, iwe imekamilika na ufaulu uongezeke kwa wanafunzi wa darasa la nne.

"Nataka shule hii ndani ya wiki mbili, darasa la wanafunzi wa chekechea liwe rafiki kwa watoto hawa wadogo kwa kuwekwa picha za aina tofauti ukutani kuhusu wanachosoma," alisema.

Alibainisha kuwa lengo la serikali kufanya hivyo ni kuweka mazingira mazuri ya ujifunzaji na ufundishaji kwa walimu na wanafunzi.

Akizungumzia suala la ufaulu kwa wanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Nkuhungu, Waziri Jafo aliagiza uongezeke na kufikia asilimia 100 ili kusiwapo mwanafunzi atakayebaki au kurudia darasa.

Awali Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nkuhungu, Benard Chanai, alisema shule hiyo ilianzishwa mwaka 1992 ikiwa na vyumba sita vya madarasa, wanafunzi 102 na walimu watatu.

Alifafanua kuwa hadi kufikia mwaka huu, ina wanafunzi 106 wa elimu ya awali na 3,646 kati ya hao wavulana ni 1,821 na wasichana 1,834 wa darasa la kwanza hadi la saba.

Alisema kwa upande wa miundombinu shule ina jengo moja la utawala, vyumba vya madarasa 24 wakati mahitaji ni 82, upungufu ni 58.

"Kwa upande wa samani, mahitaji ya madawati ni 1,216 yaliyopo ni 1,089 upungufu ni 127. Kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi wa shule hii husoma kwa awamu mbili," alisema.

Naye Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema kuwa awali shule hiyo ilikuwa na tatizo la wingi wa wanafunzi, lakini hali kwa sasa ni shwari huku akiahidi kuwa katika mfuko wa jimbo atatoa Sh. milioni 70 kwa ajili ya ununuzi wa madawati.




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Hamza Chilo, akijadiliana jambo na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, alipofanya ziara ya kikazi katika Makao Makuu ya Jeshi hilo, jijini Dodoma, jana. **PICHA: JESHI LA POLISI.**

# Polisi yatakiwa kushirikisha jamii kuondoa uhalifu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

JESHI la Polisi nchini, limetakiwa kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya dhana ya ushirikishwaji wa jamii ili kupunguza uhalifu hapa nchini.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kikazi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, jijini Dodoma.

Alilitaka jeshi hilo kuendelea kujenga ushirikiano na jamii kwa kuwa ubia huo una matokeo chanya katika kuzuia uhalifu.

Aliagiza jeshi hilo kuhakikisha linaendelea kudhibiti kikamilifu vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia katika jamii kwa kuendelea kutoa elimu kwa jamii namna ya kuzuia vitendo hivyo.

Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kumaliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia kinyume na utaratibu, badala yake washirikiane na jeshi hilo kwa kutoa taarifa ili wahusika washughulikiwe kisheria.

Akikagua jengo jipya la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Chilo aliahidi kushirikiana bega kwa bega na jeshi hilo kuboresha vitendea kazi ikiwa ni pamoja na jengo hilo kukamilika ili watendaji wake watekeleze majukumu yao katika mazingira mazuri.

Alipongeza jeshi hilo kufanya kazi nzuri ya kuendelea kudumisha amani na utulivu nchini licha ya kuwapo kwa uhaba wa vitendea kazi.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, wakati akitoa taarifa ya tathmini ya hali ya ulinzi na usalama nchini, alisema hali ya usalama ni shwari kwa kuwa uhalifu umepungua kwa asilimia 15.5.

"Kuna tatizo la kuwepo kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na uhalifu unaovuka mipaka ambao Jeshi la Polisi bado linaendelea kuyashughulikia kwa kufanya operesheni mbalimbali za kuzuia uhalifu," alisema.

IGP Sirro alisema kuwa jeshi hilo limeweka mikakati ya kupambana na uhalifu wa aina yoyote kwa kuendelea kutoa elimu ya ushirikishwaji wa jamii kwa wananchi.

Aliwataka wananchi kujiepusha na vitendo vya kihalifu na badala yake washirikiane na jeshi hilo kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili kukamatwa na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

# Viongozi wahujumu fedha za ushirika watangaziwa kiama

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI imewatangazia kiama viongozi wa vyama vya ushirika wanaohujumu fedha na mali zingine za vyama hivyo ikidai kuwa haitasita kuingilia kati na kuwadhibiti ili kuhakikisha ushirika unastawi na kuwanufaisha wanachama.

Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Collins Nyakunga, aliyasema hayo wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya (CHUTCU) ambao uliambatana na uchaguzi wa viongozi mbalimbali.

Nyakunga alisema serikali ndiyo mlezi mkuu wa vyama vya ushirika, hivyo ikitokea viongozi wa vyama hivyo wakawa wabadhirifu wataondolewa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria ili wachaguliwe wengine ambao ni waaminifu.

Alisema wakati wa uchaguzi wa viongozi wa vyama vya ushirika, wanachama wanatakiwa kuepuka kuwachagua watu wanaotoa rushwa kwa maelezo kuwa watu wa aina hiyo hawana nia ya dhati ya kustawisha vyama.

"Viongozi wa vyama vya ushirika mnapewa dhamana kubwa sana na wanachama wenu, sasa wananchi huwa wanauchukia ushirika kwa sababu ya uhuni wa wachache, sasa mmeona waliohujumu ushirika maeneo mbalimbali nchini wanavyoshughulikiwa, msije mkailaumu serikali kwamba inaingilia shughuli zenu," alisema Nyakunga.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, alisema serikali haiwezi kunyamaza kama hali siyo shwari ndani ya vyama vya ushirika na badala yake itachukua hatua ili kuvinusuru.

Alisema katika wilaya yake atahakikisha vyama vya ushirika vinastawi kutokana na kuwa na manufaa makubwa kwa wananchi na kwa serikali hasa katika usimamizi wa mazao mbalimbali ambayo yanauzwa kupitia ushirika.

Alisema endapo ushirika unaenda sawa, viongozi wa serikali hawawezi kufanya chochote na hawawezi kuonekana kwenye vyama hivyo, lakini watajitokeza pale inapotokea sintofahamu.

"Kuna baadhi ya viongozi wachache wao ni wapigaji siku zote, huwa hawapendi kuona ushirika unastawi hivyo huwa wanafanya kila mbinu ya kuudidimiza, sasa wakitokea hao ndipo serikali inapoanza kuonekana na kuchukua hatua," alisema Mayeka.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa CHUTCU, Juma Nshishi, aliiomba serikali kuwasaidia baadhi ya wakulima wa tumbaku ambao mpaka sasa hawajalipwa fedha za mauzo ya mazao yao ya msimu uliopita.

Alisema wakulima hao wanadai zaidi ya Dola za Marekani 200,000 na kwamba wamekuwa wakienda mara nyingi kwa viongozi wa CHUTCU kuomba wasaidiwe kudai fedha hizo ili waendeleze kilimo cha zao hilo mwaka huu.

"Wengine waliwakopa vibarua na wengine walikopa pembejeo kwa hiyo wasipolipwa fedha hizo inakuwa shida kwao maana na wao hawatakuwa na namna ya kulipa madeni hayo," alisema Nshishi.

Baadhi ya wakulima wa tumbaku, waliiomba serikali kuwasaidia kuongeza idadi ya kampuni zinazonunua zao hilo msimu wa mwaka huu ili kuongeza ushindani utakaowanufaisha wakulima hao.

Mmoja wa wakulima hao, Francis Kasekwa, alisema kwa sasa limebakia kampuni moja pekee linalonunua tumbaku wilayani humo, hali ambayo alidai ni hatari kwa soko la zao hilo.

Alisema endapo kampuni hazitaongezeka, wakulima wataishia kuwalaumu viongozi wao na kwamba inakuwa rahisi hata kampuni hilo kuwarubuni wakulima.

Mkoa wa kitumbaku wa Chunya unajumuisha wakulima kutoka katika wilaya mbili pacha za mikoa miwili ambazo ni Chunya yenyewe kwa upande wa Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Songwe kwa Mkoa wa Mbeya, wilaya ambazo awali ilikuwa moja.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (katikati), akitoa maelekezo kwa maofisa wa Wakala wa Majengo nchini (TBA), ambao wanasimamia ujenzi wa jengo la upasuaji na wodi ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya alipofanya ziara ya kukagua mradi huo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Busokelo waiomba serikali baraka wajenge mabweni

**Na Nebart Msokwa, BUSOKELO**

WADAU wa maendeleo wa Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wameiomba serikali iwaruhusu kujenga mabweni katika shule zote za sekondari ndani ya halmashauri hiyo ili wanafunzi wote kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne wakae shuleni.

Wanadai kuwa lengo la mpango huo ni kuinua kiwango cha elimu kwa madai kuwa wanafunzi wakikaa shuleni inakuwa rahisi kujisomea kwa uhuru tofauti na wanapotoka nyumbani ama kwenye nyumba za kupanga.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa Tamasha la kutangaza utamaduni wenye asili ya Busokelo pamoja na kuhamasisha maendeleo ambalo lilifanyika katika Mji Mdogo wa Luangwa.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Gwakisa Mwasyete, alisema wanafunzi huwa wanatumia muda mwingi kutembea njiani kutoka nyumbani kwenda shuleni na kurudi na hivyo huwa wanachoka kiasi cha kushindwa kujisomea.

Alisema vilevile wanafunzi wanaotoka nyumbani hutumia muda mwingi kucheza kuliko kujisomea tofauti na wale wanaokaa shuleni ambao muda mwingi wanakuwa chini ya usimamizi wa walimu wao.

Alisema wanao uwezo wa kujenga mabweni hayo na wanachohitaji kutoka serikalini ni ruhusa pamoja na ushirikiano kwa madai kuwa watahitaji baadhi ya wataalamu kutoka serikalini pamoja na miongozo mbalimbali ya ujenzi.

"Sh. bilioni 1.08 zinatosha kabisa kujenga mabweni kwenye shule zote za halmashauri yetu, tunachotaka ni kumaliza madaraja ya sifuri, nne na tatu kwenye matokeo ya kidato cha nne, tunataka vijana wafaulu kwa daraja la kwanza na pili," alisema Mwasyete.

Alisema serikali ilifanya vizuri kuondoa ada kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari, lakini kilichobakia kwa wazazi na wadau wengine wa elimu ni kuboresha miundombinu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Eston Ngilangwa, alisema wazo la wadau hao ni zuri na lina manufaa katika sekta hiyo na hivyo akasema amelipokea ombi la wadau hao na lazima lifanyiwe kazi kikamilifu.

Alisema wanafunzi wakikaa mabwenini inakuwa rahisi hata walimu wao kuwasimamia wakati wa masomo ya maandalizi ya jioni tofauti na wakienda kujisomea nyumbani ambako wanakutana na majukumu tofauti.

"Nitashirikiana na hawa wadau na nitawaomba ujenzi wa mabweni haya uanzie kwenye shule kubwa ambazo ni Luanga, Lufilyo, Ntaba na Shule ya Mzalendo ambazo zina idadi kubwa ya wanafunzi," alisema Ngilangwa.

# Mgogoro wakwamisha vijana kunufaika na ardhi ya serikali

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

ZAIDI ya vijana 50 wa Mji wa Rujewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wameshindwa kunufaika na ardhi ambayo walipatiwa na serikali ya wilaya hiyo miaka miwili iliyopita kwa ajili ya kilimo kutokana na kuwekewa vizuizi na matajiri wanaodai eneo hilo ni mali yao.

Mwaka 2018 Serikali ya Wilaya ya Mbarali ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, iligawa eneo lenye ukubwa wa ekari 57 katika Kitongoji cha Mdodela kilichopo Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa kwa vijana ili walitumie kwa shughuli za kilimo cha mpunga.

Vijana hao wanadai tangu wakati huo mpaka sasa hawajawahi kunufaika na mashamba hayo kutokana na kukamatwa mara kwa mara na Jeshi la Polisi hasa wanapojaribu kutaka kuyaendeleza mashamba hayo.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi, waliiomba Serikali Kuu kuingilia kati mgogoro huo kwa madai kuwa Serikali ya Wilaya hiyo imeshindwa kuwasaidia.

Baraka Mwilongo, alisema vijana hao 57 kila mmoja ana ekari moja, lakini hakuna hata mmoja aliyewahi kulima tangu walipopewa na serikali kutokana na mgogoro ambao hawamjui adui yao halisi.

Alisema Serikali ya Wilaya hiyo iliwagawia mashamba hayo kwa nia njema, lakini kwa sasa hawaoni tija ya mashamba hayo kwa sababu ya matatizo yaliyoibuka.

"Tumekuwa tukikamatwa na kupelekwa Polisi na tukifuatilia hatupati msaada wowote, tumefuatilia tumechoka, hivyo tumeona ni vema tuwaombe viongozi wa ngazi za juu serikalini, ili watusaidie tuendelee kulima mashamba yetu," alisema Mwilongo.

Naye Maria Dismas, alisema asilimia kubwa ya vijana hao wana familia ambazo walitegemea kuzilea kwa kutumia mashamba hayo, lakini kwa sasa wamekwama na hawana uwezo wa kukodi mashamba makubwa kwa ajili ya kilimo.

Alisema wanamwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, awasaidie na kwamba kama na yeye hatawasaidia wataomba hata kwa rais.

"Sisi hatuna nguvu za kupambana na wanaotuzuia ndiyo maana tunaomba msaada, sasa endapo mawaziri hawatatusaidia tutamuomba Rais Magufuli atusaidie, hatuna kwa kwenda zaidi ya hapa tulipopewa na serikali," alisema Maria.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Jangulutu, Abdul Nungwe, alikiri kushirikiana na serikali ya wilaya kuwapatia vijana hao mashamba, lakini kwa sasa ushirikiano wa kutatua mgogoro huo ni mdogo na hivyo kusababisha vijana kuendelea kupata shida.

Alisema amekuwa akithubutu mara nyingi kushughulikia mgogoro huo, lakini anakwama kutokana na kutopata ushirikiano, hivyo akadai kuwa hatua ya vijana hao kumuomba Waziri ni nzuri na huenda ikawasaidia kupata ardhi yao.



# Maalim Seif afanya ziara kujua kero utendaji kazi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, amefanya ziara kwenye Idara ya Mazingira ili kujua kero ya utendaji kazi na kubadilishana mawazo ya watendaji hao ya namna bora ya kufikia malengo ya serikali ya kuweka mazingira safi na salama.

Maalim Seif alikwenda katika ofisi hiyo, Maruhubi Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharib Unguja nakupokelewa na wakurugenzi wa ofisi hiyo wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka.

Idara ya Mazingira ni miongoni mwa zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Maalim Seif, alisema, serikali haiwezi kulipuuza suala la mazingira kwa kuwa kuyatunza ni muhimu hata kwa afya za wananchi wake.

Aliipongeza idara hiyo kwa kupambana kwa kiasi kikubwa kuondoa matumizi ya mifuko ya plastiki na kuwataka wafanyakazi wa Idara hiyo kwa kusaidiana na serikali kuangalia namna ya kuzalisha malighafi za ujenzi.

"Ni ukweli usiofichika kwamba kuchimba mchanga na mawe kunaathiri mazingira, lakini kila siku watu wanajenga majumba na wanahitaji bidhaa hizo, sasa kaeni na watafiti mwangalie ni namna gani mtazalisha nyenzo nyingine za ujenzi mbadala wa kuchimba mchanga na hayo mawe ili wananchi pia waendelee na shughuli zaoza ujenzi."

Aliwapongeza watendaji wa ofisi hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali katika suala la kuhakikisha jamii inatunza mazingira katika maeneo yanayowazunguka.

Akielezea ripoti ya utendaji kazi wa ofisi Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Sheha Mjaja Juma, alisema mpaka sasa wamedhibiti uwapo wa mifuko ya plastiki, ambayo ilikuwa kwakiasi kikubwa inachafua mazingira.

Alisema jamii imeanza kuwaelewa na kutambua umuhimu wa kutunza mazingira kwa kuwa walikuwa wanakutana na kero nyingi walipokuwa wanatoa elimu ya mazingira kwa jamii.

Alisema wamefanikiwa kuanzisha dampo kubwa la taka maeneo ya Kibele, Mkoa wa Kusini Unguja.

Katika kero zao walisema wanakutana na wakati mgumu wanapokuwa wanafanya ulinzi wa maliasili zisizo rejesheka kama vile mchanga, kifusi na kokoto kwa kuwa mara nyingi wanakutana na mapambano na wananchi ambao wanachukua vitu hivyo bila ya kufata utaraibu.

Mkurugenzi huyo alisema licha ya kupata dampo hawajafanikiwa kupata vifaa sahihi kwaajili ya kuchomea taka hizo.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, akifunua pazia kuzindua rasmi majengo ya Shule ya Assalam katika eneo la Kizimkazi, Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# SMZ kushirikiana na wadau uchumi wa buluu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, ili kuhakikisha malengo ya uchumi wa buluu yanafikiwa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, alisema hayo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, wakati wa sherehe za uwekaji jiwe la msingi na ufunguzi wa majengo ya Shule ya Assalam iliyopo Kizimkazi, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema ili kufikia malengo ya maendeleo, kunahitaji kushirikiana na kila mdau wa maendeleo hasa sekta ya elimu.

Alisema serikali ya awamu ya nane itaendelea kuwa karibu na wawekezaji wa maendeleo kwa kuwaelekeza namna ya kufuata miongozo bila ya kuvunja sheria ili kufikia malengo.

Alisema shule za kijamii ni miongoni mwa vyanzo vizuri vya maendeleo katika jamii na Wizara ya Elimu itaendelea kuwa pamoja nao kwa kuwapa mwongozo wa sera ya elimu ya Zanzibar ili kwenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wote.

Alisema uongozi wa Assalam umefanya jambo zuri kuhakikisha wanawekeza katika sekta ya elimu na ujasiriamali vijijini na wanakijiji kujiajiri wenyewe kutokana na ujuzi waliopatiwa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rashid Makame Shamsi, alisema ataendelea kusimamia maendeleo ya wilaya yake hasa katika sekta ya elimu ambayo huzalisha wataalamu wote duniani.

Nao wamiliki wa shule hiyo, Sadiki Mohammed Ali na Hatice Colak, walisema lengo la kuanzisha shule hiyo katika kijiji cha Kizimkazi na vijiji jirani ni kuhakikisha wanatoa elimu ya awali na msingi na wanasaidia wanawake, watoto, wazee pamoja na watu wenye mahitaji maalum.

Walisema wana taasisi isiyokuwa ya kiserikali ambayo inajishughulisha na masuala ya kijamii ikiwamo uchimbaji wa visima katika vijiji na kuwasaidia watu walio na hali ngumu kimaisha.

Shule ya Assalam Community Foundation imeanzishwa mwaka 2017 ili kutoa taaluma kwa wananchi wa Zanzibar hasa vijijini.

# Polisi yanasa viroba vya bangi kwenye gari

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, limekamata viroba viwili vya bangi vikiwa kwenye gari, eneo la Mtoni kwa Sharifumsha, Wilaya ya Magharibi A.

Bangi hiyo ilikutwa kwenye gari hilo aina Porte lenye namba za usajili Z.674 FY.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, ACP Awadhi Juma Haji, alisema hayo wakati akitoa taarifa za matukio mbalimbali ndani ya mkoa huo katika kipindi cha wiki moja kuanzia Januari 12 hadi 19, 2021.

Alisema tukio hilo limetokea Januari 18, 2021 majira ya saa 9:00 usiku baada ya bangi hiyo iliyokuwa imeshushwa kutoka kwenye mashua hadi askari wanafika katika eneo la tukio walikuta imeshaondoka na watu waliokuwa katika gari hilo walikimbia na kutokomea kusikojulikana na kulitelekeza gari hilo likiwa na bangi ndani.

Alisema uchunguzi wa tukio hilo unaendelea ili kuwabaini watuhuhumiwa waliohusika na tukio hilo na kuwafikisha mahakamani.

Alisema tukio lingine lilitokea Januari 17, 2021 majira ya saa 2:00 usiku eneo la Mtoni Kidatu Wilaya ya Magharibi A, mkazi wa eneo hilo, Bikombo Mussa Hassan (30), alijimwagia mafuta ya taa maeneo ya miguuni na kujichoma moto kwa kutumia kiberiti kwa nia ya kutaka kujiua baada ya kupata taarifa kutoka kwa shemeji yake kuwa mumewe kaoa mke wa pili.

Kamanda alisema mwanamke huyo aliingia chumbani kwake na kutenda kosa la kujaribu kujiua na mumewe, Hamad Harid Hassan (43), alipoingia chumbani alifanikiwa kuuzima moto huo na kumkimbiza Hospitali ya KMKM iliyopo huko Kibweni.

Alisema majeruhi huyo anaendelea na matibabu na hali yake inaendelea vizuri, huku upelelezi wa shauri hilo utakapokamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa kitendo cha kujaribu kujiua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, alibainisha tukio lingine lililotokea Januari 17, mwaka huu, majira ya saa 7:00 mchana huko maeneo ya Matarumbeta, Wilaya ya Mjini, baada ya nyumba ya Mohd Said Rashid (34), mkazi wa Matarupenda kuungua moto na kuteketeza vyumba viwili na mali iliyokuwamo ndani ya nyumba hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## NYUMBA INAUZWA

**NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA VYUMBA VIWILI INAJITEGEMEA, PLOT NA 712/1,BLOCK 46**

**MAWASILIANO 0787233272 0674927560**

## TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSTITUTE

**INATANGAZA MUHULA MPYA WA MASOMO KOZI,KILIMO,MIFUGO NA MAENDELEO YA JAMII.CHUO KIMESAJILIWA NA NACTE REG. PWF/041/ KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI. 0752761280/0767574701 AU WWW.TRACDI.AC.TZ**

## NAFASI YA KAZI

**ANAHITAJIKA RIG BORING MACHINE OPERATOR 10' INCHES REVOVER MAWASILIANO 0713 233334 0714 511696 DAR ES SALAAM**

## ANATAFUTWA DEREVA

**Anatafutwa dereva wa kike mwenye uzoefu wa kuendesha Magari Mjini Dar es Salaam. Mwenye nia na kazi hiyo apige namba 0784691605/0715691605.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**STEPHEN MANYANGU** anatangaza kupotelewa na Cheti Bodi ya usajili wa Wahandisi **(ERB)** chenye namba ya usajili **RG/C/03,** kilichotolewa mwaka **2012** pamoja na cheti cha shahada ya sayansi katika uhandisi na usanifu wa majengo,kilichotolewa na chuo kikuu cha Dar Es Salaam mwaka **2010** chenye namba **BSC(CSE)000454 .**
Yeyote atakae kiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na **STEPHEN MANYANGU** kwa simu Namba **0765945421.**
**RB NAMBA/SHY/RB/ 6880/ 2015.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**STEPHEN MANYANGU** anatangaza kupotelewa na Cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S0135-0067** kilichotolewa na baraza la mitihani Tanzania kupitia Shule ya Sekondari **MOSHI TECHINICAL** mwaka 2003, na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0155-0609** shule ya **TABORA BOYS** mwaka **2006.**
Yeyote atakae viona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na **STEPHEN MANYANGU** kwa simu Namba **0765945421.**
**RB NAMBA/SHY/RB/ 6880/ 2015**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TONNY ALBERT NYABAYAMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUBARU IMPREZA** yenye namba za usajili **T 356 DNR,** chasis namba **GHB003270** engine namba **EJ20D188468,**yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa

**CONTROL NUMBER 991081994655**

## KIAPO

Mimi **ABDALLAH KHALFAN SALIM** ambae pia natumia jina la **ABDALLAH SALUM AMRI** wa Wilayani Ngara natangaza kuwa mimi ndio mliki halali wa gari aina ya **MERCEDES BENZ** lenye namba za usajili **T.563 AKT,** Engine namba **422911017325** Chasisi namba **40393210139597.**

Kiapo hiki kimefanyika hapa Ngara na huyu ABDALLAH KHALFAN SALIM Mbele yangu mimi **MWASI J.MASINDE**

Sahihi..................................

Tarehe 28/11/2020

Cheo HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGRO**
**MAOMBI NA.256/2021.**

**TAUSI SAID KITAMBI................MLETA MAOMBI.**

**DHIDI YA**

1. **MALKIA SUPHIAN KABELWA**
2. **MOHAMED MAJUTO KATUNDU**
3. **KATUNDU TRADERS LIMITED**
4. **BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED**

**5.MABUNDA AUCTIONMART...........WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

1. MALKIA SUPHIAN KABELWA
2. KATUNDU TRADERS LIMITED

Popote walipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 26/01/2021 nyie wenyewe binafsi au mtume wawakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtohudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 16 Mwezi DECEMBER 2020.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RICHARD WILFRED KAYOMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina la **MARTIN JIDASAKA MADALO** aina ya **TOYOTA COASTER** Yenye namba za usajili **T 672 BEX.**Chassis No. **HDB510001990,** Engine No. **1HDEAA1990** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DOM/DOM/RB/33924/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi 6/2021**

Ombi la SUZAN SAIDI KARANI kuteuliwa
Msimamizi wa mirathi ya Marehemu JAMES SAIDI KARANI
KWA YEYOTE YULE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 11/02/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Tarehe 13/01/2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;20/2021

Ombi la DAVID PIUS MBWILO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SALVINA ANATORY RUYIMBA.Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/02/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/01/2021.

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT SONGEA**
**APPEALLANT JURISDICTION**
**APPEAL 9 OF 2019**

From original CR no 217 of 2018
In the district court of TUNDURU AT TUNDURU YASSIN HASSAN @MRORE
APPEALLANT
VERSUS
THE REPUBLIC…………………RESPONDENT
TO YASSIN HASSAN@MRORE OF UMOJASTREET TUNDURU 0769384326
NOTICE OF DATE F HEALING

TAKE NOTICE that the above case hs been set fixed for hearing of the appeal against conviction and sentences filed by the APPEALLANT
You are required to appeal in this court on the 10th day of FEBRUARY 2021 at 9:00 am or soon thereafter,before Hon S.C.KWSHI JUDGE
Given under my hand and the seal of the court this 25th day NOVEMBER 2020

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NYEMO FRANK KITAINDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS STAR** Yenye namba za usajili **MC 269 CDY.** Chassis **No.MD625AF71J1NO1648, Engine No.AF7NJ601623** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/4769/2021.**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Trump aondoka, ajivunia mafanikio

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, jana aliondoka madarakani, huku akitoa hotuba ya kuwaaga Wamarekani akisema katika utawala wake ameleta mafanikio makubwa.

Katika hotuba hiyo, Rais Trump hakumtaja mrithi wake Joe Biden kama mshindi wa uchaguzi uliopita, lakini alitumia dakika 20 za hotuba yake kuelezea mafanikio ya uongozi wake.

Sehemu ya hotuba hiyo Rais Trump alisema: "Tulirejesha nguvu ya Marekani nyumbani na nje ya nchi, dunia inatuheshimu tena, tulijenga uchumi imara katika historia ya dunia hii, tuliimarisha uhusiano wetu nje ya nchi hasa dhidi ya China."

**Tulifanya jambo ambalo ni muujiza wa kitabibu nalo ni chanjo. Kirusi ni kitu kibaya sana.**

"Lakini tumesababisha uwiano katika eneo la mashariki ya kati, hakuna aliyeamini na sasa eneo hilo lina mwamko mpya, najivunia kuwa rais wa kwanza kwa muda mfupi ambaye hakuanza vita vipya."

Rais Trump alisema: "Ikulu palikuwa makazi mazuri sana. Tumekuwa na miaka minne mizuri sana na tumefanikisha mengi, Tunawapenda Wamarekani na kimekuwa kitu cha kipekee."

Kadhalika, Rais Trump aligusia kuhusu janga la ugonjwa wa corona ambalo lilishika kasi katika kipindi cha miezi tisa iliyopita ya utawala wake

Rais Trump alisema: "Tulifanya jambo ambalo ni muujiza wa kitabibu nalo ni chanjo. Kirusi ni kitu kibaya sana."

Saa chache kabla ya kuondoka, Rais Trump alitoa msamaha kwa wanamuziki, Lil Wayne na Kodak Black na aliyekuwa Meya wa mji wa Detroit, Kwame Kilpatrick, huku aliyewahi kuwa mshauri wake, Steve Bannon, akitarajiwa pia kusamehewa. **DW**




Rais mpya wa Marekani, Joe Biden, ambaye aliapishwa jana kuwa rais wa taifa hilo. **PICHA: ALLIANCE**

## Nchi sita Afrika zasitishiwa haki ya kupiga kura

**WASHINGTON,** Marekani

UMOJA wa Mataifa (UN), umesitisha haki za kupiga kura kwa nchi saba kati yake sita ni za Afrika, ambazo hazijalipa deni la ada ya ushirika.

Miongoni mwa nchi hizo, ni Iran ambayo ina deni kubwa zaidi la ada ya ushiriki zaidi ya dola milioni 16.

Nchi nyingine ambazo haki zao za kupiga kura pia zimesimamishwa ni Niger, Libya, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Sudan Kusini na Zimbabwe. Nchi hizo zinatakiwa kulipa angalau kiasi maalum cha deni lao la ada ya ushiriki ili kupata haki zao za kupiga kura.

Hati ya UN ina uwezo wa kusitishwa haki za kupiga kura kwa nchi ambazo hazijalipa ada zao za miaka miwili.

Bajeti ya kila mwaka ya UN ni dola bilioni 3.2.

Muungano huu pia hutumia bajeti ya dola bilioni 6.5 kwa shughuli za kulinda amani kila mwaka.

Mwaka jana, haki za kupiga kura za nchi za Venezuela, Lebanon, Yemen, Gambia, Tonga, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Lesotho zilisimamishwa kwa sababu ya kukataa kulipa ada ya ushiriki. **TRT**

## Bill Gates anamiliki ardhi kubwa kuliko yeyote Marekani

**NEW YORK,** Marekani

MWANZILISHI wa kampuni ya teknolojia ya kimataifa ya Microsoft, nchini Marekani, Bill Gates, ameongeza zaidi ya ekari milioni moja ya ardhi kwa utajiri wake wa dola bilioni 132 na kuwa mmiliki mkubwa zaidi wa ardhi nchini humo.



Gates (pichani) alinunua zaidi ya ekari milioni moja ya ardhi katika majimbo 18 yanayoanzia Washington hadi Florida.

Miongoni mwa ardhi hizo za Gates ni pamoja na ekari 9,779 za ardhi ya kilimo na 1,109 za ardhi nyingine ya matumizi.

Bado haijulikani ni madhumuni ya bilionea huyo wa Marekani kuwekeza sana katika ardhi ya kilimo. **TRT**

## Jack Ma 'Alibaba' ajitokeza hadharani tangu mwaka jana

**Shanghai,** CHINA

MWANZILISHI wa Kampuni ya Alibaba Jack Ma alijitokeza mara ya kwanza hadharani tangu Oktoba, mwaka, jana.

Jana Ma, alizungumza na kundi la walimu kupitia video na kupunguza wasiwasi wa kutokuwapo kwake hasa kwenye kuchangia hisa kwa biashara kubwa ya e-commerce.

Uvumi juu ya mahali alipo, Ma, uliibuka baada ya habari mwezi huu kwamba alibadilishwa kushiriki kipindi cha runinga ambacho alikuwa jaji, na wakati wa kukomeshwa kwa sheria na Beijing kwenye himaya yake ya biashara iliyokuwa ikiongezeka.

Bilionea huyo, ambaye anaheshimika na ibada za nchini China, hakujitokeza hadharani tangu Oktoba 24, mwaka jana. Hiyo ni baada ya kuelezea mfumo wa udhibiti wa China.

Hadi wakati huo Ma mara nyingi alionekana hadharani, akizungumza kwenye mikutano na hafla zingine, ingawa mara chache kuliko mwaka 2019 kwa sababu ya janga la corona.

Alibaba ni kampuni ambayo msingi wake ni hisani kwa wote, katika video hiyo ya sekunde 50, Ma, aliongea akiwa katika chumba, haikujulikana chumba kilikuwa wapi. **REUTERS**

## Aliyekuwa askofu mkuu avuliwa cheo kwa uzinzi

**Kampala,** UGANDA

KANISA la Anglikana nchini Uganda limemvua cheo aliyekuwa Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Stanley Ntagali na kusitisha utendaji wa majukumu ya uaskofu pamoja na kuzuiwa kuwakilisha kanisa hilo kwa madai ya uzinzi.

Ntagali alistaafu Machi, mwaka jana baada ya kuhudumu kwa miaka 43 kama askofu.

Katika taarifa ya Januari 13, mwaka huu, kwenye tovuti ya kanisa la Anglikana mrithi wake Dk. Stephen Kaziimba, alisema, Ntagali alijihusisha na uhusiano na mwanamke mmoja aliyekuwa kwenye ndoa na hilo alilifahamu.

"Alisaliti ofisi ya askofu, kiapo alichokula wakati wa kuapishwa, na maadili mema aliyotekeleza kwa kujitolea," Dk. Kaziimba aliongeza.

Kaziimba alisema kanisa la Uganda limejitolea kuwa na uwazi pamoja na kutoa uangalizi wa uchungaji kwa wale ambao wameathirika na hali hiyo na kutoa wito wa maombi kwa wanandoa wote, kuomba msamaha na maridhiano. **DW**

# FIKAYO KUONDOKA CHELSEA




**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amethibitisha kuwa Fikayo Tomori "anaweza kwenda kwa mkopo kwa ajili ya kujiimarisha zaidi" wakati huu uhamisho wa beki huyo kwenda AC Milan ukikaribia.

Milan wameripotiwa kuwa karibu kumsajili kwa mkopo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, huku kukiwa na chaguo la kumsajili moja kwa moja, lakini 'Blues' wanatarajia kumrudisha London mwishoni mwa msimu.

Lampard alipoulizwa kuhusu hilo na waandishi wa habari alisema: "Hakuna maelezo, lakini hiyo haijathibitishwa." Mchezaji huyo wa zamani wa England, alikiri kuwa nyota huyo anaweza kuondoka Stamford Bridge kwa mkopo.

Lampard anaamini anahitaji kuondoka ili apate nafasi ya kujiimarisha zaidi.

"Sidhani kama kuna mahali tulianza kufanya vibaya kuwaendeleza wachezaji. Fikayo ni mchezaji anayekua.

"Kama kikosi tulikuwa na mabeki wa kati watano mwaka jana, na huwezi kuwachezesha wanne katika mchezo mmoja. Na unajaribu kuwa na uthabiti kwa nyakati tofauti."

Lampard amesisitiza kuwa nyota huyo amekuwa akijiimarisha, lakini kwa mahitaji ya timu sasa ipo na ziada katika mabeki watano iliyokuwa nao. Hiyo ndiyo sababu kubwa anaamini kumuacha.

# Messi afungiwa mbili, Barca yakata rufani

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imethibitisha kwamba, itakata rufani kwa mechi mbili alizofungiwa nahodha wake, Lionel Messi.

Messi alioneshwa kadi nyekundu dakika ya 121 kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la Supercopa de Espana wakati wakifungwa na Athletic Bilbao, baada ya kumpiga kwa nyuma Asier Villalibre wakati wakiwa hawana mpira, tukio ambalo lilinaswa na VAR.

Ilikuwa kadi yake nyekundu ya kwanza kuonyeshwa tangu aanze kuichezea klabu hiyo na ikiwa ni ya tatu katika maisha yake ya soka kwa kipindi cha miaka 17, akiichezea Barca na Argentina.

Barca ilipoteza kwa kichapo cha mabao 3-2 mjini Seville na kamati ya mashindano ya Shirikisho la Soka la Hispania (RFEF), jana ilitangaza kumpa adhabu hiyo Messi ya kumfungia mechi mbili.

Hiyo maana yake ni kwamba, atakosa mchezo wa Copa del Rey (Kombe la Mfalme) dhidi ya Cornella leo, Alhamisi na mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania dhidi ya Elche Jumapili, kabla ya kurudi uwanjani dhidi ya Villalibre na Athletic Januari 31, mwaka huu.

Lakini Barca imetangaza kwamba itakata rufani ya adhabu hiyo kwa RFEF haraka inavyowezekana.

Taarifa ya Barca ilisema: "Barcelona itakata rufani kwa adhabu iliyotolewa kwa Leo Messi ya kumfungia mechi mbili."







# *Solskjaer sasa kumwanzisha Diallo*

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema, Amad Diallo ameonyesha uwezo "wa kushangaza sana" kwenye mazoezi na anaweza kupewa mechi yake ya kwanza kwa Manchester United hivi karibuni.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alikamilisha uhamisho wa kutua United akitokea Atalanta, dili ambalo lilikubaliwa mwanzoni mwa Oktoba mwaka jana.

Lakini Solskjaer amevutiwa na jinsi winga huyo alivyobadilika hadi sasa na kupendekeza kuwa anaweza kuwa uwanjani kwa timu ya kwanza ndani ya mwezi mmoja.

Solskjaer hapo awali alisifu kiwango chake wakati wa mazoezi ya Diallo na alikwenda mbali zaidi kwa kusema ataanza kumpanga muda si mrefu

"Mzuri sana," alisema Solskjaer juu ya Diallo akinukuliwa na Sky Sport.

"Anaweza kushughulikia mpira, amefurahia mazoezi, hufanya tofauti katika mazoezi, ambayo ni ya kushangaza sana kwa umri wake."

Alipoulizwa kama inaweza kuwa wiki nne au tano hadi kuanza kwake, Solskjaer aliongeza: "Inaweza kuwa haraka kuliko hiyo, hakika ametulia vizuri."

HABARI MICHEZO

# Drinkwater atimkia Uturuki

**ISNTANBUL,** Uturuki

KIUNGO wa Chelsea, Danny Drinkwater, amejiunga na timu ya Kasimpasa ya Ligi Kuu ya Uturuki, Super Lig, kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu, baada ya kukosa nafasi kwenye kikosi cha Frank Lampard.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 30, hajacheza kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea kwa miaka miwili na nusu, huku mara ya mwisho alionekana akiwa amevalia uzi wa Blue Agosti 2018.

Amecheza mara 23 kwa miamba hiyo ya London Magharibi, lakini ni tangu walipopoteza kwenye Ngao ya Jamii mbele ya Manchester City mwaka 2018 alipotokea benchi.

Drinkwater amewahi kutolewa kwa mkopo kwenye klabu za Burnley na Aston Villa msimu uliopita, na msimu huu alijiunga na wachezaji wenye umri chini ya miaka 21 na chini ya miaka 23 wa Chelsea, ili kukidhi haja ya kucheza angalau kila mwishoni mwa wiki.

Drinkwater ambaye bado ana mkataba wa miezi 18 pale Stamford Bridge, aliichezea England mara tatu, aliisaidia Leicester City kushinda taji la Ligi Kuu msimu wa 2015-16, lakini ameshindwa kutamba akiwa na Chelsea aliyojiunga nayo kwa pauni milioni 35, mwaka 2017.

Kipindi akiwa kwa mkopo huko Burnley na Aston Villa, hakuwa na nafasi, akiwa amecheza mara mbili tu.




# ZIDANE AWAKATAA ALABA, MBAPPE



**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amejibu juu ya uvumi wa taarifa za usajili wa nyota wa Bayern Munich, David Alaba na mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe.

Alaba atakuwa nje ya mkataba mwishoni mwa msimu huu wa 2020-21 na Jumatatu gazeti la nchini Hispania, Marca, lilidai kwamba, makubaliano ya kutua katika klabu hiyo ya LaLiga kwa muda wa miaka minne tayari yamefikiwa.

Mlinzi huyo hodari ambaye baba yake ni mshauri katika klabu ya Real Madrid, hajajibu chochote tangu ahusishwe na mabingwa hao wa LaLiga.

Alipoulizwa juu ya uvumi unaoendelea kwenye mkutano na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa Copa del Rey (Kombe la Mfalme) dhidi ya Alcoyano jana Jumatano, Zidane hakuwa tayari kuongelea jambo hilo.

"Naelewa unataka kuniuliza kuhusu swali hili juu ya mchezaji ambaye si wa klabu yetu, lakini nipo hapa kuongelea mchezo wa Jumatano (jana)," alisema.

"Naelewa kuna mnachokitaka, lakini sitajibu, sasa mimi na timu yangu tunaangalia mchezo uliopo mbele yetu."

Bosi huyo wa Real Madrid alitoa majibu hayo hayo alipoulizwa juu ya mshambuliaji wa PSG, Mbappe kama angependa kuwa na mchezaji huyo kutoka Ligue 1.

Alisema:"Samahani tayari nimeshasema tunaangalia mchezo wa Jumatano kama nilivyo wajibu juu ya Alaba."

# *Mandzukic asajiliwa rasmi AC Milan*

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan imetangaza kukamilisha usajili wa mshambuliaji, Mario Mandzukic.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia amejiunga na miamba hiyo ya soka la Italia kwa mkataba wa miezi sita, huku kukiwa na kipengele cha kumwongezea mwaka mmoja.

Mandzukic anatua Milan kama mchezaji huru, baada ya kuachana na klabu ya Al-Duhail ya nchini Qatar ambayo aliitumikia kwa mwaka mmoja akifunga bao moja kwenye michezo saba aliyocheza.

Kabla ya kujiunga na Al-Duhail, mshambuliaji huyu aliitumikia Juventus kwa miaka mitano na sasa anarudi tena kwenye Serie A akiwa na Milan ambapo atavaa jezi namba tisa.

Kusajiliwa kwa Mandzukic ni sehemu ya mkakati wa klabu hiyo kuongeza nguvu kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Italia, ambapo kwa sasa wanaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi tatu dhidi ya wapinzani wao Inter Milan.



**HABARI MICHEZO**

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LAMPARD AFUNGUKIA KIPIGO CHA CHELSEA

**●●● Kitu pekee tunachoweza kufanya ni kupita kwenye wakati huu, kujituma kwa bidii ili...**

**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza kwamba anaweza kukabiliana na presha wakati huu Chelsea ikizidi kuonyesha kiwango kibovu, baada ya juzi Jumanne kufungwa mabao 2-0 na Leicester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

**Mabao kutoka kwa Wilfred Ndidi na James Maddison yaliipeleka Leicester kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, pointi tisa dhidi ya kikosi cha Chelsea ambacho sasa kimeshinda mechi mbili tu kati ya nane zilizopita za ligi.**

Timu hiyo ya Lampard imepitwa pointi tano kutoka kwenye nne bora, huku pointi zake 29 za sasa zikiwa ni chache zaidi ambazo Chelsea imewahi kuzipata ikiwa katikati ya msimu tangu msimu wa 2015-16, wakati Leicester waliposhinda taji na Blues hao ambapo walimaliza nafasi ya 10.

Alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu majaliwa yake baada ya mchezo huo, Lampard alijibu: “Niliulizwa kabla, naelewa, ni matarajio ya klabu hii.

“Ni timu inayoendelea kukua, lakini siwezi kufanya chochote kwenye vitendo. Nilichukuwa kazi hii nikijua tutakuwa na nyakati ngumu.

“Tunatakiwa kupambana. Kila kitu kilikuwa cha kawaida Desemba, na sasa hali si sawa. Nipo vizuri na naweza kuikabili presha.”

Kuhusu kiwango cha timu yake, Lampard aliiambia BBC Sport: “Tulikuwa kwenye nafasi nzuri sana Desemba, wa pili kwenye ligi tukipitwa pointi mbili kutoka kileleni.

“Pengine tunatakiwa kuamka upya. Kuna njia moja tu ambayo ni kujituma kwa bidii. Leo Leicester walikuwa bora kuliko sisi.

“Ni suala tunaloliangalia. Ni wakati ambao hatuna furaha, klabu nyingine zimeshawahi kuwa kwenye wakati kama huu.

“Kitu pekee tunachoweza kufanya ni kupita kwenye wakati huu, kujituma kwa bidii. Kitu cha muhimu ni wachezaji kurudi kwenye kiwango chao. Hakuna namna nyingine.

“Wachezaji wanatakiwa kuendelea kunyanyua vichwa vyao juu na kufungua macho na kujaribu kuangalia michezo iliyopo mbele yetu.”

## ZISIKUPITE

### ATLETICO KUMFUNGA SIMEONE

ATLETICO Madrid inamtaka kocha wake, Diego Simeone kusaini mkataba mpya, ambao utamuweka klabuni hapo hadi mwaka 2024. ***(AS)***

### SPURS KUMSAJILI INGS

TOTTENHAM Hotspur inafikiria kumsajili mshambuliaji wa Southampton na England, Danny Ings mwenye umri wa miaka 28. ***(Eurosport)***

### LUKAKU HAITAKI MAN CITY

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 27, hana mpango wa kujiunga na Manchester City. ***(Express)***

### BUENDIA AGOMEWA ARSENAL

ARSENAL imeambiwa kwamba, kiungo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 24, Emi Buendia hataondoka pale Norwich City wakati wa dirisha hili la usajili la Januari. ***(Independent)***

### WEST HAM KUMKOSA LABORDE

KLABU ya Montpellier imekataa ofa kutoka West Ham kwa ajili ya kumsajili straika Gaetan Laborde mwenye umri wa miaka 26. ***(Guardian)***

### SOUTHAMPTON NA MISHAHARA

KOCHA wa Southampton, Ralph Hasenhuttl, amesema hali ya kifedha ya klabu hiyo haiwezi kuhimili kulipa mishahara mikubwa kwa wachezaji muhimu kama Danny Ings. ***(Mirror)***

### ALABA BADO LULU ULAYA

LIVERPOOL na Barcelona hazijakata tamaa ya kumsajili mlinzi wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, licha ya Real Madrid kuwa karibu kukamilisha usajili huo. ***(Sport1)***

### MEDINA ATAKIWA MAN

MANCHESTER United inaanda pauni milioni 11 kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa Lens na Argentina, Facundo Medina mwenye umri wa miaka 21. ***(La Voix du Nord)***

### BARELLA AWANIWA EPL

LIVERPOOL na Tottenham zinaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa Inter Milan na Italia, Nicolo Barella mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

### NICE YAMTOSA LINGARD

NICE imepooza mpango wake wa kutaka kumsajili kwa mkopo kiungo wa Manchester United na England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28. ***(Sky Sports)***

### DELE BADO ANUKIA PSG

KIUNGO wa Tottenham Hotspur na England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, anajiamini atakamilisha haraka dili lake la mkopo la kwenda Paris St-Germain, Januari hii. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Namungo yaanza kuwasoma Waangola

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema ameanza kuwapeleleza wapinzani wao, Primeiro de Agosto ya Angola kwa kuangalia mechi zao mbalimbali walizocheza hivi karibuni ili kuanza kujipanga kuwakabili.

Morocco aliliambia gazeti hili kikosi chake kina kazi kubwa ya kuhakikisha kinajiimarisha kuelekea mchezo huo wa mtoano wa Kombe la Shirikisho Afrika na tayari ameshaanza kufanyia kazi upungufu uliyopo katika kikosi chake.

Kocha huyo alisema wanahitaji kuimarisha ubora wao ili kujitengenezea mazingira ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya kimataifa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara pia.

"Nimepata nafasi ya kuangalia baadhi ya michezo waliyocheza, tunatakiwa kujipanga vizuri kila idara kwa ajili ya kukabiliana na wapinzani wetu, si timu nyepesi, wazuri kila sehemu kikubwa kwangu ni kuhakikisha nafanyia kazi upungufu uliopo hasa katika safu ya ushambuliaji, tunahitaji kutafuta ushindi pamoja na kuimarisha ulinzi," alisema Morocco.

Namungo FC wanatarajia kuanzia ugenini ambapo mechi yao inatarajiwa kuchezwa Februari 12, mwaka huu na marudiano yakiwa mwishoni mwa mwezi huo.

## Ihefu yajipanga kujinasua mkiani

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ihefu FC unatarajia kukutana kwa ajili ya kupanga mikakati ya kuhakikisha timu hiyo inaondoka katika nafasi iliyopo kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Tayari mabosi wa timu hiyo, walishakutana na Kocha Mkuu, Zuberi Katwila, kupokea programu zake za kiufundi zitakazosaidia kutimiza malengo waliyojiwekea.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Ihefu, Juma Nyauba, alisema kikao hicho kitaangalia ripoti ya usajili uliofanywa katika kipindi cha dirisha dogo na kuandaa utekeleza wa mahitaji mengine muhimu yatakayowasilishwa.

Nyauba alisema wanahitaji kujikomboa kwa kufanya vizuri katika mechi za mzunguko wa pili na hawajakata tamaa kwa sababu nafasi ya kurekebisha makosa bado ipo.

Ihefu FC yenye pointi 13 inashika mkia katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kushinda michezo mitatu, kutoka sare mechi nne na kufungwa michezo 11.

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS HAZIKAMATIKI

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens na timu ya Yanga Princess zimeendelea kufanya vema katika ligi hiyo kwa kutoa vichapo katika mechi zilizochezwa juzi kwenye viwanja tofauti hapa nchini.

**Simba Queens iliyokuwa ugenini ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya wenyeji Mlandizi Queens na kuifanya ifikishe pointi 23 na kuendelea kubakia katika nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo, lakini ikiwa na mchezo mmoja mkononi.**

Mabao ya Simba Queens katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani, yalifungwa na Asha Djafari na Oppa Clement.

Vinara Yanga Princess wenyewe walitoa kichapo cha bila huruma cha mabao 7-0 kwa TSC, shukrani kwa wafungaji Aisha Khamis aliyefunga manne, Amina Ally akipachika wavuni mawili, huku Philomena Daniel akifunga la saba katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Kwa matokeo hayo, Yanga Princess imefikisha pointi 28 ikifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 24 ambao na wao juzi wakiwa ugenini waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Alliance Queens.

Mlandizi Queens inashika nafasi ya nane ikiwa na pointi 11 na imecheza michezo nane ikishinda mitatu, sare mbili na kufungwa mitatu, TSC ikiwa katika nafasi ya tisa imecheza michezo nane ikishinda miwili sare mmoja na kufungwa mitano, huku ikiwa na mechi mbili mkononi.

Ruvuma Queens wao wako katika nafasi ya sita wakiwa na pointi 12, baada ya kucheza michezo tisa ikishinda mitatu, sare tatu na kufungwa mitatu na Tanzanite SC ipo nafasi ya saba na pointi zake 12 kutokana na kushinda michezo minne na kufungwa sita.

Kigoma Sisterz yenyewe imecheza michezo tisa na inashika nafasi ya 10, ikiwa imeshinda moja, sare moja na kufungwa saba hivyo kujikusanyia pointi nne, huku Mapinduzi Queens ikishika nafasi ya 11 na Es Unyanyembe inaburuza mkia baada ya kupoteza mechi zote12 ilizocheza.

Ligi hiyo inayodhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) ilitarajiwa kuendelea tena jana jioni katika viwanja mbalimbali hapa nchini.

MAZOEZI...



Wachezaji wa Timu ya Fedha FC, wakiwania mpira wakati wa mazoezi katika Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Majimaji kuwaenzi mashujaa wake*

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

UONGOZI wa timu ya Soka ya Majimaji inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, umepanga kuanzisha Tamasha la Makumbusho ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji wa Mkoa wa Ruvuma, imeelezwa.

Ofisa Michezo wa Mkoa wa Ruvuma, Anzawe Chaula, jana alisema lengo la kuanzisha makumbusho hayo ni kuwaenzi waasisi wa timu hiyo dhamira ikiwa ni kuwaweka vijana pamoja.

"Marehemu Dk. Lawrence Gama ambaye wakati huo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, alishirikiana na wakazi wa Songea kuiendesha (timu), kwa ubia kati ya serikali na wananchi, hatua iliyochangia kuanzishwa kwa kamati maalumu ya kusimamia maendeleo ya mpira ya mkoa (KAMASUPA), ambayo ilipewa jukumu la kutafuta pesa pamoja na kusimamia timu," alisema Chaula.

Aliongeza kuwa, mwaka 2000 wanachama wa klabu hiyo katika kikao cha pamoja na uongozi wa mkoa, waliridhia timu iondolewe rasmi chini ya uendeshaji wa mkoa na kupelekwa kwa wanachama, lakini bahati mbaya timu hiyo ilishuka daraja.

Alisema wanahitaji kuona timu hiyo inafanya vizuri na hatimaye kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara huku ikiendelea kuzalisha wachezaji tegemeo kwa nchi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Majimaji ambayo ilianzishwa mwaka 1978, ilikuwa na mafanikio mbalimbali, ambapo msimu wa 1986/87, ilibeba ubingwa wa Kombe la Muungano huku msimu wa 1998/99 ikicheza michuano ya Klabu Bigwa Afrika kwa sasa Ligi ya Mabingwa Afrika na kutolewa na Al Ahly ya Misri.

Baadhi ya wachezaji nyota walioibuliwa na timu hiyo ni pamoja na Abdallah Kibadeni, Iddi Pazi, Peter Tino na Madaraka Suleiman ambao walitamba miaka ya nyuma, huku hivi karibuni ikiwatoa Ditram Nchimbi anayecheza Yanga na Jaffar Mohamed aliyeko Namungo FC.

Michezo

Alhamisi Januari 21, 2021

Nipashe



HABARI UK.20

## Messi afungiwa mbili, Barca yakata rufani

# Matola atetea kipigo cha Taifa Stars

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA msaidizi wa timu ya soka ya Tanzania, Taifa Stars, Selemani Matola, amesema wamepoteza mechi kwa mabao 2-0 dhidi ya Zambia kwa makosa ya kimpira tu na wala si kuzidiwa kama inavyoelezwa na baadhi ya mashabiki.

Akizungumza nchini Cameroon baada ya mechi iliyochezwa mjini Limbe, Matola alisema walifungwa bao la penalti ambayo ilitokana na makosa ya kimchezo, ambayo ndiyo yalisababisha hata kupatikana kwa bao la pili.

"Tumepoteza mechi, wachezaji wetu walicheza vizuri sana vipindi vyote viwili, siyo kipindi kimoja tu kama inavyosemwa. Tatizo ni kwamba lilikuwa ni kosa tu la bahati mbaya mpira ulimgonga Shomari Kapombe mkononi ikapatikana penalti, wakaitumia, hivyo ndiyo iliyosababisha wachezaji wetu wahamaki na kutaka kurudisha bao, lakini waliacha mianya ambayo Zambia waliitumia kutuadhibu bao la pili," alisema Matola ambaye ni mchezaji wa zamani wa Taifa Stars.

Hata hivyo, alisema watarekebisha makosa hayo ili kushinda kwenye mechi inayofuata.

Nahodha wa timu hiyo, Shomari Kapombe, alisema tatizo kubwa lilikuwa ni kupungua umakini kipindi cha pili.

"Kipindi cha kwanza tulicheza vizuri sana, lakini cha pili kuna sehemu tulipoteza umakini tukaruhusu kufungwa mabao mawili," alisema na kuongeza kuwa sasa wameyaacha na wanaangalia mechi inayokuja. Yalikuwa ni mabao ya Collin Sikombe kwa mkwaju wa penalti na Emmanuel Chibula yaliyoiangamiza Stars.

Timu hiyo ambayo iko Kundi D, inatarajia kucheza mechi ya pili siku ya Jumamosi dhidi ya Namibia ambayo nayo ilikubali kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Guinea.

**MATESO...**



James Maddison (kulia) akimtesa kipa wa Chelsea, Edouard Mendy, baada ya kuachia shuti lililomshinda na kujaa wavuni hivyo kuiandikia Leicester bao la pili wakati ikishinda 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England, iliyopigwa Uwanja wa King Power juzi. Bao la kwanza lilifungwa na Wilfred Ndidi. **Habari Uk 22. PICHA: MTANDAO** .

# KAZE: YANGA SASA RAHA TU

## Majembe mapya yampa jeuri ya makombe Jangwani, huku akimtaja Carlinhos kuwa kwa sasa...

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa furaha! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, ambaye tayari ameshaipa klabu hiyo ubingwa mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa mwaka huu ambayo yalifanyika mapema mwezi huu visiwani Zanzibar.

Yanga ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 44, wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Simba wenye pointi 35, lakini wamecheza mechi tatu pungufu ukilinganisha na watani zao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema anaamini wachezaji walioongezwa katika kipindi cha dirisha dogo, wataisaidia timu yake kufikia malengo waliyojiwekea msimu huu.

Kaze alisema sasa ana kikosi imara ambacho kina uwezo wa kupambana na timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa sababu ndio mashindano makubwa waliyonayo pamoja na michuano ya Kombe la FA.

Kocha huyo alisema alilazimika kuongeza 'majembe' katika kikosi chake kwa sababu anafahamu wazi hakuna mechi nyepesi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA ambayo inachezwa kwa mtindo wa mtoano.

"Malengo yetu msimu huu ni kuchukua ubingwa, ninajua wanachokitaka mashabiki wa Yanga, nimekuja kuwapatia furaha hiyo, malengo yetu ni kuwa na msimu yenye furaha, tumejiandaa na tumejipanga kupambana na timu zote, hatutadharau mchezo wowote," alisema Kaze.

Aliongeza amekuwa akiwapa mbinu tofauti wachezaji wake ili kucheza kwa malengo na kwa sasa kila mmoja anatekeleza maelekezo kwa kiasi kikubwa.

"Wachezaji wangu wanazidi kuwa bora na imara kila siku zinavyokwenda, tunakumbushana mbinu mbalimbali kulingana na aina ya timu tunayokutana nayo, kikubwa ni kuendelea kupambana kuchukua pointi katika kila mechi ili tufikie malengo," Kaze aliongeza.

Kuhusu kiungo nyota wa timu hiyo, Carlos Carlinhos, alisema anatarajia kurejea kikosini kuungana na wachezaji wenzake baada ya majeraha yake kuendelea vizuri.

Alisema kwa sasa kiungo huyo yupo tayari kuanza mazoezi mepesi, ikiwamo ya kwenda Gym, lakini akiendelea kufuata programu nyingine chini ya usimamizi wa madaktari kabla ya kuungana na wenzake atakapokuwa fiti kuanza kuingia uwanjani.

"Nilimwondoa kwenye kikosi kilichoshiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi ili apone kikamilifu, muda ambao umemsaidia kupona kwa kiwango kikubwa, kwa sasa atarejea kuipigania timu katika mechi za mzunguko wa pili ambao ndio fainali," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >